Ripoti hii ni matokeo ya utafiti watoto 500, wenye umri kati ya miaka 7 - 14 kutoka mikoa kumi ya Tanzania Bara. Utafiti huu ni wa kwanza wa aina yake kwa Tanzania, unatoa uelewa wa watoto kwa masuala yanayohusiana na elimu: huduma za shule kama vile afya, upatikanaji wa maji na chakula, vitabu vya kiada, walimu, nidhamu, gharama za ziada na matamanio ya watoto katika kuboresha elimu.

Katika sehemu ya pili ya utafiti, watafiti walitafuta maoni ya watoto juu ya wajibu wao katika jamii, hasa michango yao kijamii na kiuchumi kwa familia zao na jumuiya, matamanio yao ya kupata taarifa, njia rasmi na zisizo rasmi za kuwasikiliza, na mategemeo yao ya baadaye.

ISBN 978-9987-615-32-2

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Uelewa wa Watoto wa Tanzania Kuhusu Elimu na Nafasi Yao katika Jamii
## Maoni ya Watoto Mwaka 2007

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page i

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



# Uelewa wa Watoto wa Kitanzania Kuhusu
## Elimu na Nafasi Yao katika Jamii
## Maoni ya Watoto Mwaka 2007

Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA:
Kundi la Utafiti na Uchambuzi na
Kundi la Wataalamu wa Mawasiliano,
Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

Desemba 2007

Maelezo na nakala zaidi za taarifa hii zinaweza kupatikana:

**Sekretariati ya MKUKUTA, Kitengo cha Kupunguza Umaskini,**
**Wizara ya Fedha na Uchumi**
S.L.P. 9111, Dar es Salaam Tanzania

Simu: +255 (22) 2111174/6

Barua pepe: mkukutamonitoring@gmail.com
ps@mof.go.tz

Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz

Pia kutoka Sekretariati ya Kundi la Utafiti na Uchambuzi:

**Research on Poverty Alleviation (REPOA),**
Kitalu 157, Mtaa wa Mgombani, Regent Estate,
S.L.P. 33223, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 (22) 2700083 / 0784 555 655
Baruapepe: repoa@repoa.or.tz
Tovuti: www.repoa.or.tz

Imechapishwa na: REPOA kwa niaba ya Kundi la Utafiti na Uchambuzi
Ubunifu wa michoro umefanywa na Total Identity
© Kundi la Utafiti na Uchambuzi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2008

ISBN: 978-9887-615-32-2

UNICEF Tanzania ilifadhili mradi huu

Kwa marejeo taja: Kundi la Utafiti na Uchambuzi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2008), 'Uelewa wa Watoto kuhusu Elimu na Nafasi Yao Katika Jamii. Maoni ya Watoto Mwaka 2007'. Dar es Salaam, Tanzania

Maneno muhimu: Tanzania, watoto, haki za mtoto, utafiti wa uelewa, ustawi wa jamii, elimu, ushiriki, mawasiliano, kujifunza

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page iii

# YALIYOMO

Orodha ya Majedwali . . . . . . . . . . iv

Shukrani . . . . . . . . . . **v**

**Muhtasari: Wanachokisema Watoto** . . . . . . . . . . **vii**

**1. Utangulizi** . . . . . . . . . . **1**

**2. Methodolojia** . . . . . . . . . . **3**
- 2.1 Uhusiano na utafiti wa 'Maoni ya Watu' . . . . . . . . . . 3
- 2.2 Uchaguzi wa sampuli . . . . . . . . . . 3
- 2.3 Kufanya utafiti na watoto wakiwa washiriki . . . . . . . . . . 7
- 2.4 Utayarishaji wa ripoti hii . . . . . . . . . . 7

**3. Vipengele Muhimu** . . . . . . . . . . **9**
- 3.1 Eneo la kijiografia . . . . . . . . . . 9
- 3.2 Kipato cha wazazi . . . . . . . . . . 9
- 3.3 Umri wa washiriki wa utafiti . . . . . . . . . . 9
- 3.4 Jinsia . . . . . . . . . . 10

**4. Maoni ya Watoto kuhusu Shule, Ufundishaji na Kujifunza** . . . . . . . . . . **11**
- 4.1 Huduma shuleni . . . . . . . . . . 11
- 4.2 Vitabu . . . . . . . . . . 12
- 4.3 Walimu . . . . . . . . . . 13
- 4.4 Nidhamu na adhabu . . . . . . . . . . 16
- 4.5 Michango . . . . . . . . . . 18
- 4.6 Je, hali inaboreshwa? Nini kifanyike ili elimu iwe bora? . . . . . . . . . . 19

**5. Maoni ya Watoto kuhusu Nafasi Yao katika Jamii** . . . . . . . . . . **21**
- 5.1 Watoto ni wachangiaji hai kijamii na kiuchumi . . . . . . . . . . 21
- 5.2 Taarifa wanazozihitaji watoto na vyanzo wanavyovitegemea . . . . . . . . . . 21
- 5.3 Nani huwasikiliza watoto na kwa nini? . . . . . . . . . . 24
- 5.4 Matarajio ya baadaye . . . . . . . . . . 26

**6. Hitimisho la Ujumla** . . . . . . . . . . **31**

**Kiambatanisho: Maelezo ya Methodolojia** . . . . . . . . . . **35**

Marejeo . . . . . . . . . . 41

# ORODHA YA MAJEDWALI


| | | |
|---|---|---|
| Jedwali la 1 | Kiwango cha umaskini kutokana na sampuli | 4 |
| Jedwali la 2 | Sampuli ya watoto kwa maeneo, kiwango cha umaskini na umri wao | 6 |
| Jedwali la 3 | Mapendekezo ya watoto kuhusu namna ya kuboresha elimu | 19 |
| Jedwali la 4 | Taarifa wanazozihitaji watoto | 22 |
| Jedwali la 5 | Vyanzo vya taarifa vinavyotumika na watoto | 23 |
| Jedwali la 6 | Matarajio ya watoto kuhusu kazi | 27 |
| Jedwali la 7 | Mwainisho wa kazi wanazotarajia kuzifanya watoto | 28 |

# SHUKRANI

Utafiti huu, unaojulikana kama utafiti wa 'Maoni ya Watoto' na ulibuniwa kujazilizia utafiti wa 'Maoni ya Watu'. Utafiti wa Maoni ya Watu wa mwaka 2007 ni utafiti mkubwa uliofanywa kama sehemu ya mfumo wa ufuatiliaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Matokeo makuu ya utafiti wa Maoni ya Watoto yalijumuishwa katika ripoti kuu ya 'Maoni ya Watu' - hata hivyo, chapisho hili la ziada linatoa maelezo ya kina zaidi ya utafiti huu wa 'Maoni ya Watoto.'

Utafiti huu ni muhimu sana kwa Tanzania kutokana na mawanda yake na taarifa zilizokusanywa; na pengine ni wa kwanza au miongoni mwa tafiti chache za aina hii zilizowahi kufanywa katika nchi za Kiafrika zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara. Watoto wetu ni taifa la kesho; serikali inakusudia kuendeleza tafiti za aina hii, hususan katika eneo muhimu la haki za mtoto.

Watu wengi walichangia kukamilika kwa ripoti hii na michango yao inatambuliwa kwa kuwashukuru.

Wanachama wa Programu ya REPOA ya Utafiti wa Watoto wanapewa shukrani kwa kubuni mradi huu na msaada wao wa kiufundi katika kipindi chote cha utekelezaji. Uchambuzi wa matokeo ya utafiti na utayarishaji wa ripoti ulifanywa na Kate Dyer, Derrick Mbelwa, Francis Omondi na Zubeida Tumbo-Masabo.

Wakuu wa Mikoa, Maafisa Elimu wa Wilaya, Maafisa Tendaji wa Kata, Waratibu Kata wa Elimu na walimu wakuu wa shule katika wilaya zilizokuwa kwenye sampuli yaani Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Singida, Mtwara, Lindi, Mwanza, Shinyanga, Iringa na Rukwa wanashukuriwa kwa msaada wao wakati wa utafiti wa uwandani.

Serikali inaishukuru UNICEF kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi huu, ikiwemo kuchapisha ripoti hii.

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, shukrani za pekee ziwaendee watoto walioshiriki katika utafiti, wakiwemo wale wawakilishi kutoka Mabaraza ya Watoto kwa Manispaa za Temeke na Kinondoni ambao walishiriki katika mjadala wa vikundi wakati wa kuchagua mada za utafiti.

voc 30-9-08 :Layout 1  10/9/08  2:48 PM  Page vii

# MUHTASARI Wanachokisema Watoto

Utafiti huu ni wa kwanza wa aina yake kwa Tanzania. Watoto mia tano wenye umri kati ya miaka 7 mpaka 14 kutoka maeneo kumi tofauti mijini na vijijini na wenye hali tofauti kijamii na kiuchumi walikuwa sehemu ya mradi wa utafiti shirikishi uliofanyika kama sehemu ya utafiti wa 'Maoni ya Watu'. Ufuatao ni muhtasari wa matokeo hayo:

## Uelewa

**Watoto hutazama mambo kwa namna tofauti na watu wa wazima**

Masuala ambayo watafiti watu wazima waliyaona kuwa ni vipengele tofauti vya utafiti (kusoma shule na nafasi ya watoto katika jamii), watoto waliona kwa ujumla zaidi kama yote ni sehemu ya suala hilo hilo moja. Masuala ambayo watu wazima kwa kawaida huona kuwa yameunganika sana, kwa mfano faini kama aina ya adhabu, watoto walikuwa na mtazamo tofauti. Kwao, faini ni njia nyingine ya kutozwa mchango wa kifedha.

**Watoto wana mawazo yanayoweza kutoa uelewa unaofaa kuzingatiwa na watu wazima**

Ingawa watoto wanaweza wakawa na ufahamu mdogo wa baadhi ya masuala - kama vile viwango vya michango vinacholipwa shuleni, (hii yawezekana ni kwa sababu ya umri wao), wanaweza kuweka masuala katika vipaumbele tofauti na watu wazima. Watoto waliofanyiwa utafiti walilipatia umuhimu mkubwa suala la mawasiliano kati ya nyumbani na shuleni, na kwa upande wa walimu wao kuwa na taswira nzuri kwa jamii zao (badala ya kuiona jamii kama ya walevi tu). Umuhimu wa masuala haya kwao ulionekana mkubwa kuliko uzito uliowekwa na baadhi ya watu wazima katika masuala haya.

Pia walibainisha mkinzano wa wazi uliopo kati ya mitaala ya shule ambayo husisitiza lishe bora, na ukweli kwamba wao hawapewi chakula shuleni.

## Elimu

**Kwa kuzungumza na watoto ilionekana kwamba sehemu kubwa ya kujifunza shuleni ni kupokea tu kutoka kwa walimu, kutegemea sana kunakili maandishi kutoka ubaoni na kwenye vitabu vya kiada**

Watoto wengi walisisitiza kuwa walimu wawe na mwandiko mzuri ubaoni, ikionyesha jinsi ilivyo muhimu kwa watoto kwamba waweze kusoma mwandiko huo.

Vitabu vya kiada vinathaminiwa na kupendwa sana na watoto hawa, lakini vilevile ni chanzo cha kuwavunja moyo, kwani ingawa kwa ujumla kuna ongezeko la usambazaji wa vitabu vya kiada, bado vitabu ni vichache sana kulinganisha na mahitaji yaliyopo. Watoto wangependa kujisomea vitabu kwa muda wao wenyewe, lakini kwa ujumla vitabu hukusanywa mwishoni mwa kila kipindi.

**Watoto wanazijua sifa ambazo mwalimu anatakiwa kuwa nazo**

Mwalimu anapaswa kuwa mtu ambaye kweli anataka kufundisha, anayewapenda watoto, anakuwa na bidii na kuhakikisha wanafunzi wanaelewa. Ilionekana kwenye utafiti kuwa baadhi ya watoto walikuwa na walimu wenye sifa hizi.

Kuhusu walimu, watafiti walikuta baadhi ya matendo bora kama vile kuwafanya wanafunzi wenye matatizo ya kuona kuwa sehemu ya shule ya kawaida.

**Kila shule iliyokuwa kwenye sampuli iliripoti matatizo yanayoonyesha walimu kutokutimiza wajibu wao wa msingi kimkataba, au kuwa na viwango vya chini vya weledi**

Walimu kushindwa kuhudhuria vipindi ni tatizo kubwa. Watoto walizungumzia kuhusu walimu ambao waliotoa vitini lakini hawakuvielezea, au waliwaambia tu kuwa kama hawakuelewa wakawaulize wanafunzi wa madarasa ya juu.

**Kanuni za adhabu ya viboko hazifuatwi** kwa shule karibu zote. Hofu ya adhabu ya viboko - inayosababishwa, kwa mfano, na walimu wanaokuwa na fimbo darasani - ilielezwa na watoto kuwa ni kikwazo kikubwa katika kujifunza.

Kwa ujumla, mchakato wa kujifunza katika **mazingira ya shule unaonekana kuwabana wanafunzi** kufuata wanayoyasema walimu kama 'amri zilizowekwa' kwa ajili ya watoto ambao kwa kiwango kikubwa kazi yao ni kuzifuata tu. Watoto walioshiriki katika utafiti huu walionyesha kuwa hawakuwahi kufundishwa/kujifunza kwa mbinu shirikishi.

Mawasiliano kati ya shule na wazazi yalikuwa hafifu.

**Michango ya hali na mali hutozwa katika shule zote** zilizokuwa katika sampuli ya utafiti, na watoto husimamishwa masomo kwa kushindwa kuilipa.

Watoto walikuwa na maoni mbalimbali walipoulizwa kuhusu hali ya elimu kama ilikuwa bora zaidi miaka ya nyuma kabla ya mwaka 2007 ambapo utafiti huu ulifanyika. Watoto wengi zaidi walionyesha kwamba njia bora zaidi ya kuiboresha elimu ni kuongeza usambazaji wa nyenzo za ziada, ikiwa ni pamoja na miundombinu, walimu, na vifaa vya shule. Vilevile walitaka wawe na walimu bora zaidi, mtaala mpana zaidi, na huduma nyingine shuleni (kama vile huduma za afya).

Watoto wa Dar es Salaam walioshiriki katika utafiti huu walidai kwa ujasiri kwamba kwa kuongeza juhudi zao binafsi katika masomo na kuwasikiliza walimu na wazazi itasaidi pia kuboresha elimu yao.

## Ushiriki katika Jamii

**Watoto ni washiriki hai kiuchumi na kijamii** na hufanya kazi mbalimbali ambazo hunufaisha familia na jumuiya, au huwasaidia watu wazima ambao walipaswa wazifanye kazi hizo, na wajibu huu huanza tangu wakiwa katika umri mdogo.

## Mawasiliano

Watoto walidhani wazazi huwasikiliza kwa njia isiyo rasmi, na maoni ya jumla ni kuwa **mawasiliano ni finyu kwa kiasi kikubwa** - matatizo yanayohusiana na shule yalitajwa mara kwa mara - ingawa hii pia inaweza kuwa ni kwa sababu utafiti ulifanyika katika muktadha wa shule.

Watoto walionyesha kuwa wana **mambo mengi wanayoyapenda na hupata taarifa kutoka vyanzo vingi mbalimbali**. Kando na nyumbani, familia na mwasiliano ya ana kwa ana, radio ni muhimu sana kwao.

**'Njia rasmi' za kuwasikiliza watoto ni duni.** Hali inayoonekana kuhusu walimu ni kwamba mtindo wao wa elimu unajikita kwa mwalimu badala ya mwanafunzi; kazi ya walimu ni kuelezea vizuri ili maarifa husika yaeleweke badala ya kuwawezesha watoto kwa uhuru zaidi kuielewa dunia wanayoishi.

'Kusikiliza' siyo sifa waliyonayo walimu, zaidi ya kusikiliza maswali machache ya wanafunzi wanayoyajibu darasani japokuwa wanafunzi katika shule moja walisema kuwa wangependa kutoa maoni yao kuhusu masuala yanayohusu elimu.

Shule moja tu kwenye sampuli ya shule kumi za msingi ilikuwa na baraza la shule lililo hai. Watoto wanapokuwa wanawakilishwa kwenye kamati za shule, japokuwa hii ni kwa nadra sana, mawazo ya watoto ni kwamba maoni yao hayatiliwi maanani. Pale ambapo hawana uwakilishi wa moja kwa moja, wanafunzi huwa hawajui lini mkutano ulifanyika na nini kilijadiliwa.

Sehemu pekee ambayo inawezekana ni tofauti katika suala hili ni misikitini na makanisani ambapo inaonekana watoto wanapewa nafasi pana zaidi ya kushiriki. Hata hivyo, hili lilionekana dhahiri katika eneo moja tu la utafiti. Hakukuwa na asasi zisizo za kiserikali au asasi za kijamii katika maeneo ya utafiti, kwa hiyo watafiti hawakuweza kupima kama hizi 'sekta mpya' zinawapa watoto fursa zaidi za kusikika.

voc 30-9-08 :Layout 1  10/9/08  2:48 PM  Page ix

## Matarajio Yao ya Baadaye

Watoto wana matarajio mbalimbali kuhusiana na kazi zao za badaye. Zaidi ya nusu ya sampuli walionyesha kuwa wanataka kuhudumu katika elimu na tiba. Wachache, zaidi ya 10% walitaka kushiriki shughuli za uongozi wa nchi kwa namna fulani, kama rais, waziri, mbunge, mkuu wa mkoa au wilaya. Chini ya 10% walivutiwa na jeshi au ulinzi na tena zaidi kidogo ya 10% walitamani kujiunga na sekta ya uzalishaji kama wakulima, mafundi (ufundi stadi au ufundi sanifu) au wafanya biashara.

## Hitimisho

Ndani ya hoja hizi mahususi kuna ujumbe wa wazi. **Watoto walifurahia kushirikishwa katika utafiti huu, na waliona kuwa walijifunza kwa kutoa maoni yao** na kwa jinsi ambavyo watafiti waliwashirikisha.

Wakati mwingine, kama itakavyoripotiwa katika chapisho hili, waliamua kuchukua hatua maalum na kuwajibika kwa mambo yaliyojitokeza katika mjadala, na ambayo yalionekana kwao kuwa siyo haki - wakionyesha jinsi gani kujifunza kwa pamoja na ushiriki mpana kijamii unavyoweza kukuzwa.

Watoto wanaona vizuri mikanganyiko iliyoko kati ya mtaala unaowafundisha umuhimu wa maji safi na lishe bora na kile wanachokipata shuleni. Mara nyingi maoni na hoja zao mahususi ni muhimu kwa watunga sera na watu wa mipango, na hii ni sababu mojawapo ya kuendelea na tafiti za aina hii juu ya 'Maoni ya Watoto' wakati wote.

**Matokeo ya utafiti huu yana kipimo cha utu kinachowapa changamoto watu wazima wote, iwe wazazi na/au weledi wanaofanya kazi na watoto:**

- **Watoto wanataka kusikilizwa na kutambuliwa.**
- **Wanataka kufundishwa na walimu wanaopenda watoto, wanaopenda kufundisha na wenye bidii.**
- **Watoto wanataka wasikike.**

# SURA 1 Utangulizi

Ni kawaida katika maendeleo kwamba mawazo ya 'wanaonufaika', yaani maoni ya watu yanahitaji kuzingatiwa katika upangaji na ufuatiliaji. Watoto ni watu pia. Ukweli kwamba karibu nusu ya Watanzania wana umri wa chini ya miaka 18[1], ikikadiriwa kuwa ni karibu watoto milioni 18[1], unashawishi kudadisi mitazamo ya watoto na vijana. Zaidi ya hayo utafiti huu unachukuliwa kuwa ni mchango muhimu kwenye utafiti wa maoni ya watu, utafiti ambao uliwashirikisha watu zaidi ya 7,000 wanaoishi Tanzania bara, ambao ulifanyika kwa wakati mmoja mwaka 2007[2] (taarifa zaidi zipo katika sura ya 2).

Hata hivyo, watoto, siyo tu kwamba ni watu wanaokua, bali pia mikabala mbalimbali inatakiwa kutumika ili kuwaelewa watoto. Hii ndio sababu kuu ya Utafiti wa Maoni ya watoto, ambao waandishi wa rasimu ya ripoti hii wameyapa kichwa kidogo cha habari, *'Kujifunza Kuwasikiliza Watoto',* kwa sababu zoezi lenyewe kwa watafiti lilikuwa ni mchakato wa kujifunza.

**Kwanini 'Kujifunza Kuwasikiliza Watoto', Watafiti Walikuwa Wanajifunza Nini?**
Methodolojia ya utafiti huu ni ya pekee kwa Tanzania; ikitumia zana za ukusanyaji takwimu za idadi na stahilifu pamoja na sampuli za vikundi ya watoto viliyochaguliwa kwa uangalifu ili kupata uwakilishi kwa nchi nzima. Ni mara ya kwanza maoni ya watoto yametafutwa kwa mpangilio makini kama huu. Watafiti nchini Tanzania wanajaribu kuiga mbinu bora zinazokubalika kimataifa wanapotafiti maoni ya watoto kwa lengo la kujifunza namna ya kusikiliza mawazo yao.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa watoto wana mengi ya kusema yanayojaziliza matokeo ya tafiti zingine, na ungekuwa na manufaa ya wazi kwa watunga sera na watu wa mipango pamoja na kwa wazazi, walimu na watu wengine wanaofanya kazi na watoto, kujifunza kutokana na kile wanachokisema watoto. Watoto wanahitaji kusikilizwa na kushirikishwa - huu ni ujumbe ulio dhahiri kutoka kwenye utafiti huu - changamoto kwa 'wakubwa zao' ni kutafuta njia za kufanya hivyo.

Mojawapo ya matokeo ya utafiti huu ni kwamba njia rasmi za kuwasikiliza watoto ni duni kwa ujumla: watoto wanatarajiwa <u>kusikiliza</u> zaidi ya wanavyotarajiwa <u>kushiriki</u> katika mijadala ya masuala yanyohusiana na maendeleo yao au ya jamii zao. Matokeo ya hali hii siyo dhahiri, ingawa yawezekana hayasaidii kabisa kujenga watu wazima wanaowajibika kuwalea na katika misingi ya kidemokrasia. Kwa upande mwingine, kuwasikiliza ni mwanzo wa kukuza ushiriki wao, na hivyo kwa kuendeleza kuwasikiliza watoto tunahamasisha ushiriki wao zaidi.

## Kwa nini Tunahitaji Maoni ya Watoto?

Zaidi ya hoja kwamba 'watoto ni watu pia', na hoja zinazotumiwa kuelezea manufaa ya ushiriki wa watu wazima zinahusika pia kwa watoto kwa uzito ule ule. Kuna mambo mawili yanayothibitisha sababu za kuelekeza tafiti kwa watoto:

1. Watoto wana haki ya kusikilizwa katika masuala yanayowaathiri wao - hii inatetewa katika Mikataba ya Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Mtoto (UNCRC au CRC)[3]. Nyingi kati ya ibara 54 za UNCRC zinahusu kuwaheshimu na kuwajumuisha watoto, huku msisitizo maalum ukiwa kwenye maslahi mazuri ya mtoto na kuendeleza usawa na kutokubaguliwa. Kwa kuwa Tanzania imeridhia Mikataba ya Haki za Mtoto, kutafiti maoni ya watoto ni sehemu ya kuheshimu vipengele vya makubaliano haya.

---

[1] Mwaka 2004 Tanzania ilikuwa na idadi ya watu karibu milioni 37.6, kati ya hao milioni 18.8 (takriban 50%) walikuwa chini ya miaka 18.

[2] Ambao ni sehemu ya Mfumo wa Usimamizi wa MKUKUTA, na unalenga kupata mawazo ya watu kuhusu utekelezaji wa MKUKUTA na utendaji wa serikali kwa ujumla.

[3] Office of the High Commissioner of Human Rights (2003). *Convention on the Rights of the Child.* http://www.unhchr.ch/html/menu3/b/k2crc.htm. [Ilisomwa tarehe 23 January 2008

2. Tayari watoto wanashiriki katika jamii kama washiriki hai, na siyo tu "raia wanaosubiri wakati wao - wakiwa na hamu ya kutimiza miaka 18"[4]. Kwa kawaida huchukuliwa kuwa ni wapokeaji tu wa huduma za jamii, hasa afya na elimu, lakini kiuhalisia wakati mwingine hufanya maamuzi yao binafsi ya kutumia hizo huduma au la. Wanaathiriwa na mazingira ya jamii wanamoishi, na pia wanafanya maamuzi na ni washirika wa kiuchumi ambao mara nyingi huchangia vizuri kwenye kipato cha familia na ustawi wake. Hivyo kuelewa mitazamo yao na vipaumbele vyao kuna manufaa katika kujaribu kuboresha hali ya maisha ya familia na jumuiya, na ubora wa programu na sera.

Katika muktadha wa Kitanzania, tafiti na habari zinazowahusu watoto kwa kusudi la mipango hazitoshelezi kabisa. Kuna kiasi kikubwa na taarifa za kitakwimu kuhusu huduma zinazotumiwa na watoto zinazopatikana kupitia mfumo wa kukusanya data mara kwa mara, hasa katika afya na elimu ambako watoto ni watumiaji wakubwa wa huduma hizo. Hata hivyo, uchambuzi wa data hizi[5] huishia kuonyesha uhusiano baina ya masuala mbalimbali badala ya kuelezea sababu za mahusiano hayo. Wakati mwingine hauwapi watunga sera na watu wa mipango maelekezo ya kutosha kuhusu hatua zinazotakiwa kuchukuliwa - kama vile, ni aina gani ya matumizi ya fedha inasaidia katika kuandikisha wanafunzi wengi na kuwezesha kuendelea na masomo shuleni: kuwa na walimu zaidi, kuwekeza zaidi kwenye miundombinu, walimu bora, na/au uwepo wa chakula shuleni? Kama watumiaji wakubwa wa huduma hizi, watoto na vijana wana nafasi nzuri ya kutoa maoni yanayofaa.

## Uchaguzi wa Mada za Utafiti

Kwa kuzungumza na watu mbalimbali, wakiwemo watoto kulisaidia kubainisha masuala muhimu ya utafiti:

1. Elimu na Kujifunza;
2. Afya, ikiwemo afya ya uzazi, na
3. Nafasi ya watoto katika jamii.

Kwa kuzingatia kuwa saa mbili mpaka tatu ni kipindi cha muda unaotosha kufanya kazi na kikundi cha watoto, iliamuliwa kuwa masuala mawili ndiyo yashughulikiwe. Nafasi ya watoto katika jamii iliendelea kusisitizwa kuwa ni muhimu katika kuelewa jinsi watoto wanavyojiona, jinsi maamuzi yanavyofanyika, na jinsi uraria unavyopatikana. Elimu ilibaki kuwa mada ya utafiti kwa sababu ni kiungo muhimu kati ya utafiti huu na utafiti wa 'Maoni ya Watu' uliokuwa unafanyika kwa wakati mmoja; na kwamba watoto ni watumiaji wakubwa wa huduma hizi zinazotolewa na serikali.

Mada juu ya afya haikufanyiwa kazi kwa sababu ilihofiwa kuibua masula nyeti, hasa yanayohusiana na haki ya kutunza siri za watoto na usalama wao, ambapo muda na rasilimali tulizokuwa nazo zisingetosha kuyafanyia kazi. Kwa mfano, ilidhaniwa kwamba baadhi ya masuala yanayoweza kuibuka katika mijadala yangefaa kujadiliwa vizuri katika vikundi vya jinsia moja, pamoja na kubadilisha zana za utafiti kwa vikundi vya umri tofauti ili kuyajadili masuala kwa njia sahihi badala ya kuwaacha watoto wakihatarishwa zaidi au wamechanganyikiwa. Ni matumaini ya timu ya watafiti kwamba bado kuna nafasi kwa ajili ya tafiti za kuchunguza jinsi matatizo ya afya yanavyoweza kutatuliwa.

---

4 Jeremy Beechman (2001) akinukuliwa katika Unicef (2006). *'Involving the Children and Young People in Planning, Implementation, Monitoring and Evaluation.'*

5 Kwa mfano, Ophelia Mascarenhas (2004). *'What We Know About Children In Tanzania Based On A Review Of Studies'* REPOA (2005) *'Vulnerable Children in Tanzania and Where they are: Report to Unicef'*.

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 3

# SURA 2 Methodolojia

## 2.1 Uhusiano na Utafiti wa 'Maoni ya Watu'

Utafiti huu, unaojulikana kama utafiti wa 'Maoni ya Watoto' ulibuniwa kujaziliza utafiti wa 'Maoni ya Watu'. Maoni ya Watu 2007 ni utafiti mkubwa uliofanyika kama sehemu ya Mfumo wa Usimamizi wa Umaskini wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Kundi la Utafiti na Uchunguzi, ambalo ni moja ya vikundi vya Mfumo wa Usimamizi wa Umaskini, iliipa REPOA kazi ya kufanya utafiti wa Maoni ya Watu. Wakati zana za utafiti kwa ajili ya Maoni ya Watu zikiandaliwa, ikaonekana wazi kuwa kuna fursa ya kuuhusisha na Programu ya REPOA ya Utafiti wa Watoto[6] . Programu hii ya utafiti tayari ilikuwa na mipango ya kufanya utafiti bunifu kwa kutumia methodolojia inayozingatia vigezo vinavyopima ubora na idadi kuhusu watoto, wakati utafiti wa Maoni ya Watu ulikuwa unalenga watu wazima wenye umri wa miaka 25-60, pamoja na kiasi kidogo cha wazee (wale wenye miaka zaidi ya 60) na vijana wenye umri wa miaka 15-24. Maoni ya vijana yalitafutwa hususan kuhusiana na elimu na njia za kujipatia riziki.

Wakati zana za utafiti kwa ajili ya utafiti wa Maoni ya Watu zikiandaliwa[7], waandaaji walitambua kuwa utafiti utakuwa na thamani zaidi kama ukilenga vikundi ya umri mdogo zaidi, kwa sababu inakadiriwa zaidi ya 50% ya Watanzania wana umri wa chini ya miaka 18. Zaidi ya hayo taarifa za serikali kuhusu upatikanaji wa huduma za shule, kwa mfano, zinaweza kujaziliziwa na watumiaji wa huduma hizo.

Hata hivyo, ilitambuliwa kuwa kutegemea watoto wadogo kujibu hojaji yenye maswali mengi kama ambavyo watu wazima watajibu kusingeleta manufaa makubwa. Umri uliopendekezwa kwa ajili ya utafiti wa watoto - miaka 7 mpaka 14, ulimaanisha kuwa umakini wao utakuwa kwa kipindi kidogo na kutakuwa na viwango tofauti vya ustadi wa lugha, hivyo kufanya matumizi ya njia za kawaida za utafiti kuwa ngumu. Kwa watoto kushiriki kikamilifu katika mradi wowote wa utafiti wanahitaji zana za utafiti zinazojali umri wao na kiwango cha uelewa. Vile vile ushiriki katika utafiti lazima uwe wa kufurahisha na wa kuleta uzoefu unaohamasisha kwa watoto. Jambo hili lilifanikiwa, ukizingatia tathmini ya watoto kuhusu ushiriki wao[8].

Hivyo ilikubaliwa kujaribu methodolojia kwa watoto wadogo ili kujaziliza utafiti wa Maoni ya Watu kwa maana ya kujadili baadhi ya masuala yanayofanana kwa lengo la kupata matokeo ambayo yatasaidia kupata mwelekeo kutoka kwa watoto wa kuanzia miaka saba mpaka kwa watu wazima.

## 2.2 Uchaguzi wa Sampuli

Ukubwa wa sampuli ulipangwa kuwa wa watoto 500. Hii ilikuwa ni 10% ya sampuli ya utafiti wa Maoni ya Watu, kiasi ambacho kilikuwa sawa kwa kuwa methodolojia ilikuwa inajaribiwa. Utafiti ulifanyika katika mikoa ile ile ya utafiti wa Maoni ya Watu, hivyo hii ilimaanisha watoto 50 kwa kila mkoa.

Kwa ushauri wa watakwimu, zilichaguliwa wilaya ndani ya mikoa ambayo ilitoa mtawanyiko wa mapato, kama ulivyopimwa kwa kiwango cha umaskini binafsi wa watu - umaskini mkubwa, kiasi na mdogo[9], pamoja na kuenea kwake vijijini, maeneo mchanganyiko na kata za mijini, kama zilivyoainishwa kwenye sensa ya mwaka 2002.

---

6 Wahusika wa Programu ya Utafiti wa Watoto inayoratibiwa na REPOA: Kate Dyer, Derrick Mbelwa, Francis Omondi na Zubeida Tumbo-Masabo, Mikala Lauridsen, Carol Watson, Rakesh Rajani, Theresa Kaijage, Valerie Leach, Rose Mwaipopo, Ophelia Mascarenhas, Amandina Lihamba, Rehema Tukai and Alice Rugumyamheto.

7 Kwa kutumia njia ya msisitizo ikiwahusisha Kamati ya Wataalamu, Washauri na wafanyakazi wa REPOA na baadhi ya AZISE za kitaifa na kimataifa. Brian Cooksey, Rose Mwaipopo na Blandina Kilama walitoa mchango wa kiufundi ulioweka sawa maswali ya utafiti.

8 Imeelezwa kwenye hitimisho sehemu ya 5.3

9 Kutoka kwenye kazi ya kubainisha umaskini, iliyoko kwenye Poverty and Human Development Report 2005.

Kutokana na hili mikoa na wilaya zifuatazo ziliainishwa:

**Jedwali 1: Kiwango cha Umaskini kutokana na Sampuli**

| Kiwango cha Umaskini | Mijini | Mchanganyiko | Vijijini |
|---|---|---|---|
| **Kikubwa** | Mkoa wa Mwanza:<br>Wilaya ya Geita | Mkoa wa Iringa:<br>Wilaya ya Mufindi | Mkjoa wa Lindi:<br>Wilaya ya Lindi vijijini |
| **Wastani** | Mkoa wa Singida:<br>Wilaya ya Singida Mjini | Mkoa wa Mtwara:<br>Wilaya ya Mtwara Vijijini | Mkoa wa Shinyanga:<br>Wilaya ya Maswa<br>Mkoa wa Rukwa:<br>Wilaya ya Sumbawanga Mjini |
| **Kidogo** | Mkoa wa Dar es Salaam<br>Wilaya ya Kinondoni | Mkoa wa Tanga:<br>Wilaya ya Tanga Mjini | Mkoa wa Arusha:<br>Wilaya ya Arusha Mjini |

Kata ziliainishwa kwa kuzingatia kuwa zilikuwa na maeneo ya vijijini, mchanganyiko au mijini. Hata hivyo, uchaguzi wa kata wakati mwingine uliathiri picha ya wilaya nzima. Hivyo, wakati kwa ujumla Wilaya ya Geita ina eneo lenye kiwango kikubwa cha umaskini, kata iliyochaguliwa ilikuwa na watu ambao walikuwa na uchumi mzuri zaidi. Vivyo hivyo, wakati Kinondoni kwa ujumla ni eneo lenye kiwango kidogo cha umaskini, na licha ya baadhi ya kaya zenye kipato kikubwa maeneo ya jirani, shule zilionekana kuwa na watu wenye kipato kidogo. Kwa kiasi fulani maeneo yaliyochaguliwa kwa kuzingatia kuwa yameshiriki pia kwenye utafiti wa Maoni ya Watu, ilikupunguza mzigo wa za ziada wa maandalizi waliyokuwa nayo watafiti wa Maoni ya Watu na kuwezesha kuhusianisha taarifa kati ya tafiti hizi mbili. Matokeo ya mwisho yalionyesha kwamba watafiti walifanikiwa kugawanya viwango kwa kipato/umaskini na tabia tofauti za kijiografia katika maeneo kumi ya utafiti.

Maelezo ya kina juu ya sifa za kila shule yanafuata, japo majina yamehifadhiwa. Zaidi ya hayo, taarifa za shule zimetolewa kwa uchache, ili kuepuka urahisi wa kuitambua shule inayohusika.

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 5

**Wilaya ya Geita, Mwanza**

Shule ipo kando kando ya barabara. Ina eneo kubwa na ina zaidi ya wanafunzi 1,000, na hivi karibuni imegawanywa katika shule ndogo mbili. Eneo lipo ndani ya uzio, ni safi na imepandwa maua vizuri. Aidha ina majengo mapya mengi pamoja na shule ya awali.

**Manispaa ya Singida, Singida**

Shule ipo katikati ya mji, na ina wanafunzi zaidi ya 900. Eneo la shule halina uzio na njia kadhaa zinakatisha katika yake.

**Manispaa ya Arusha, Arusha**


Shule hii ipo nje ya mji, na kuna nyumba chache sana zinazoizunguka. Baadhi ya wanafunzi hutembea zaidi ya kilometa kumi kwenda shule. Eneo la shule limewekwa katika hali ya usafi, kuna bustani za majani yaliyozungukwa na miti mifupi. Eneo linalozunguka shule halina uoto wowote na limesafishwa na upepo. Baadhi ya vyumba vya madarasa vina madirisha ya vioo na majengo yote kwa ujumla yanaridhisha, japokuwa sakafu zilikuwa za vumbi na mashimo. Wanafunzi kwa ujumla walivaa vizuri wakiwa na soksi na viatu na masweta mekundu kama sehemu ya sare za shule.

**Manispaa ya Tanga, Tanga**

Shule ipo karibu na barabara ya Tanga-Dar es Salaam. Baadhi ya majengo yake yalijengwa miaka ya 1950 kwa kutumia matofali ya kuchoma, lakini kwa sasa yapo katika hali mbaya kwa kukosa ukarabati. Hii ni pamoja na nyufa kubwa na paa zinazovuja. Aidha, kuna baadhi ya majengo mapya na mazingira yametunzwa vizuri, kuna bustani za maua na miti. Shule pia ina wanafunzi wasioona wanaoishi ndani ya eneo la shule. Wanaonekana kwa kiasi kikubwa kuwa ni sehemu ya shule na wanakubalika kwa wanafunzi na walimu pia. Uwepo wao ulibadilisha kwa kiasi fulani methodolojia ya utafiti kwa kuwa zana za kuonyesha zisingeweza kutumika.

**Maswa, Shinyanga**

Watoto wengi wanaishi mbali sana na shule na hivyo hawawezi kurudi nyumbani mchana kula chakula. Kuliwahi kuwa na mpango wa kutoa chakula shuleni lakini msaada wa mfadhili ulikwisha na huduma hiyo ikasitishwa, japokuwa kuna majadiliano ya kurudisha tena huduma hiyo. Watafiti walishuhudia 'gwaride la shule' baada ya chakula siku mojawapo ya utafiti. Wanafunzi walitembea kuzunguka shule wakiimba na kuongozwa na viranja na mamonita. Jambo hili lilipendwa sana na wanafunzi na liliwapatia hamasa ya kusoma kwa bidii.




**Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam**

Shule ipo katika eneo la makazi ambayo hayajapimwa na imezungukwa na baadhi wa wakazi wenye uwezo mkubwa. Hata hivyo, miundombinu - barabara, maji na maeneo ya wazi, ni mibovu. Kuna umeme kwenye ofisi ya mkuu wa shule tu. Upatikanaji wa maji siyo wa uhakika. Mabomba mengi ya maji yamepasuka, hivyo eneo la shule lililo upande wa barabara limefurika maji. Majengo ya shule ni ya zamani, sakafu ni ya vumbi na madawati hayatoshi kwa wanafunzi wote. Vyoo ni vipya na visafi, lakini hakuna maji. Mandhari ya shule ni nzuri, lakini shule haina nafasi ya kutosha wala viwanja vya michezo kwa sababu eneo hilo limejengwa shule nyingine. Kwa maneno mengine, shule mbili zipo katika eneo moja ambalo lilipaswa kuwa la shule moja.

**Sumbawanga Mjini, Rukwa**

Shule hii ipo mbali na mji wa Sumbawanga. Shule ina shamba ambamo wanafunzi hufanya shughuli za kilimo na mavuno yake huchangia katika gharama za uendeshaji wa shule kama vile kununua vitabu. Katika shule hii wazazi hawakuwa wamesoma barua ambayo iliwaomba ruhusu ya watafiti kufanya utafiti huu, badala yake walikuja shuleni kwa kudhani kuwa wameitwa kwenye mkutano. Mwalimu Mkuu aliongea nao na kuwaomba waondoke. Huu ni mfano mzuri wa matatizo ya mawasiliano kwa maandishi na wa wazazi kudhani kuwa barua yoyote inayotoka shuleni inamaanisha wao wanatakiwa kwenda shuleni.

**Wilaya ya Mufindi, Iringa**

Shule imejengwa karibu na barabara ya Iringa/Mbeya, karibu na ofisi ya kata. Shule ina eneo dogo ambalo linavutia kwa kuwa limepandwa maua. Madarasa yamejengwa vizuri yakiwa na milango yenye makufuri. Wakati watafiti walipoitembelea shule ilikuwa imefungwa kwa ajili ya likizo, isipokuwa kwa madarasa ya juu waliokuwa wana masomo ya ziada na watoto wa shule ya awali. Mwalimu Mkuu alifanya mpango maalum wa kuwaita wanafunzi walioteuliwa kwa ajili ya utafiti.

**Mtwara Vijijini, Mtwara**

Shule ipo karibu na barabara inayoelekea kwenye mpaka wa Msumbiji. Kwa ujumla, shule ipo katika hali nzuri ikiwa na vyoo vya kutosha kwa wavulana na wasichana. Kiwango cha kufaulu mtihani wa mwisho wa kumaliza shule ya msingi ni kizuri. Matatizo yanayoikumba shule ni pamoja na uhaba wa maji unaosababisha matatizo ya kiafya. Baadhi ya wazazi waliripotiwa kuwa hawaungi mkono jitihada za shule, lakini kamati ya shule ni bora kuliko zingine nyingi kwa sababu walikuwa wamenunua sanduka la huduma ya kwanza kwa ajili ya shule kwa kutumia fedha zao wenyewe badala ya fedha za shule.

**Lindi Vijijini, Lindi**

Shule iko njia ya kwenda Mtwara. Kuna zaidi ya wanafunzi 900 na kiwango cha kufaulu mtihani wa mwisho wa kumaliza shule ya msingi ni kizuri. Shule haina uzio na ina upungufu mkubwa wa walimu na majengo. Shule inahudumia vijiji kadhaa vilivyopo mbali; wanyama wa porini ni tishio kwa wanfunzi wanaokwenda shule. Kwa mujibu wa wanafunzi, mwaka 2006, kijiji kimoja katika kata hiyo ilipoteza watu 25 kwa kushambuliwa na simba. Shule ina miradi yake ya kujipatia kipato.

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 6

**Jedwali la 2: Sampuli ya Watoto kwa Maeneo, Kiwango cha Umaskini na Umri wao**

| Eneo la Utafiti | Sifa Halisi za Shule | | Umri 7-10 | | | Umri 11-14 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mkoa/Wilaya** | **Eneo** | **Kipato** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** |
| Arusha, Terat | Kijijini | Kidogo | 13 | 12 | 25 | 13 | 12 | 25 |
| Tanga, Tanga Urban | Karibu na mji | Kidogo | 8 | 17 | 25 | 10 | 15 | 25 |
| DSM, Kinondoni | Mjini | Kidogo | 11 | 13 | 24 | 12 | 14 | 26 |
| Lindi, Lindi Rural | Kijijini | Kikubwa | 10 | 13 | 23 | 12 | 14 | 26 |
| Mtwara, Mtwara Rural | Karibu na mji | Wastani | 12 | 14 | 26 | 14 | 12 | 26 |
| Iringa, Mufindi | Karibu na mji | Kikubwa | 13 | 14 | 27 | 12 | 13 | 25 |
| Singida, Singida Urban | Mjini | Wastani | 12 | 13 | 25 | 13 | 12 | 25 |
| Rukwa, Sumbawanga | Kijijini | Wastani | 13 | 12 | 25 | 16 | 14 | 30 |
| Shinyanga, Maswa | Kijijini | Wastani | 13 | 12 | 25 | 12 | 13 | 25 |
| Mwanza, Geita | Mjini | Kikubwa | 12 | 13 | 25 | 14 | 15 | 29 |
| | | **Idadi** | **117** | **133** | **250** | **128** | **134** | **262** |
| **Jumla ya Sampuli** | | | | | | | | **512** |

Shule za msingi zilipendekezwa kuwa mahali pa kuanzia kwa sababu taarifa rasmi zinaonyesha kuwa katika maeneo mengi ya nchi, idadi kubwa ya watoto angalau wameandikishwa shuleni - ingawa hii siyo lazima imaanishe kwamba wote hawa huwa wanahudhuria shule. Aidha kujikita kwa watoto wa umri wa shule ya msingi kulifanywa kwa lengo la kujaziliza utafiti wa Maoni ya Watu ambao ulikuwa unauliza maswali ya vijana wa umri wa miaka 15-24. Wakati umri rasmi wa watoto wa shule za msingi ni miaka 7-13, inajulikana vizuri wanafunzi wengi wa madarasa ya juu wana umri mkubwa zaidi ya umri huo uliopangwa kwa kiwango hicho cha elimu, (kanuni za shule zinataka watoto waanze kwenda shule wakiwa na umri wa miaka saba). Hivyo utafiti ulijikita kwa wale wenye umri wa kati ya miaka 7-14. Hawa waligawanywa katika vikundi viwili kwa umri yaani, miaka 7-10 na 11-14, kwa kuzingatia kuwa kukaribiana kiumri kutasaidia kuwa na mjadala wa kina wakati wa majadiliano ya vikundi maalum.

Katika ngazi ya shule washiriki wa utafiti walipatikana kwa kuchukua sampuli iyo na mpangilio maalum. Hii ilitumiwa kwa kiasi kikubwa[10] na wafatifi wa utafiti mkubwa wa Maoni ya Watu[11]. Watafiti walitumia daftari la mahudhurio, kwa msaada wa walimu kuhakikisha kuwa watoto walio nje ya kiwango cha umri kilichowekwa hawaingii kwenye sampuli.

Kulikuwa na tatizo kubwa la watoto ambao hawasomi shule. Uzoefu ulionyesha kwamba kuwafikia hawa kwa njia nzuri na kwa uwakilisha mzuri ni changamoto kubwa. Pale ambapo kuna mpango maalumu wa masomo kwa watoto waliokosa elimu ya msingi[12], pangeweza kuwa njia muafaka ya kuwafikia watoto ambao hawasomi, lakini mpango huu haukuwepo katika maeneo mengi. Watoto waliopelekwa katika vituo vya watoto wa mitaani hawakuwa sampuli nzuri ya kuwawakilisha watoto ambao hawasomi, na tayari ni eneo ambalo limefanyiwa utafiti sana. Pia kuwaomba msaada Walimu Wakuu au viongozi wa vijiji ili kuwapata watoto ambao hawasomi kulisababisha kuletewa watoto waliomaliza shule za msingi ambao hawakupata fursa ya kuendelea na elimu ya juu. Watoto hawapaswi kutosoma shule, hivyo

[10] Hata hivyo katika baadhi ya maeneo sampuli ilichanguliwa na watafiti wa Maoni ya Watoto kwa sababu utafiti wa Maoni ya Watu haukufika katika maeneo hayo.

[11] Dionice Boay, Afisa Elimu wa Manispaa ya Kinondoni, aliwezesha zoezi la utafiti kwa baadhi ya shule za msingi katika Manispaa ya Kinondoni. Watafiti wenyewe walikuwa Rose Beatus, John Kiango, Agnes Gabriel, Edwiga Temba, Albert Budondi, Irene Mboya, Latifa Rashid, Gertrude Venance na Ally Manjasi.

[12] Hujulikana kwa kifupi cha Kiswahili, MEMKWA.

viongozi wa vijiji na watu wengine wa nje wanaofanya jitihada za kuwatafuta mara zote hukumbana na vikwazo vingi. Hivyo iliamuliwa kutowashirikisha watoto ambao hawasomi shule kwenye sampuli ya watoto 500, lakini kutoa muda zaidi kwenye kila eneo la utafiti kujaribu kuwafikia hawa watoto katika maeneo mabayo wanaweza kuwa (mathalan wakiteka maji, wakinywesha mifugo, kwenye vituo vya mabasi) na kujaribu kuwahusisha kwenye mjadala usio rasmi kuhusu masuala ya utafiti wa Maoni ya Watoto, na kutumia maoni yao kama nyongeza kwenye matokeo ya utafiti mkubwa.

Hata hivyo, kiutendaji hili halikuwa rahisi. Changomoto zifuatazo zilijitokeza: tatizo la usafiri, ugumu wa mawasiliano ikiwa na maana kwamba kwa baadhi ya maeneo watafiti wa Maoni ya Watoto walifika kabla ya watafiti wa Maoni ya Watu, ruhusa ya wazazi haikupatikana, kulikuwa na haja ya kutumia muda kuelezea utafiti kwa walimu, kiasi kwamba muda wa ziada ulihitajika ili kuhakikisha kuwa utafiti unaendelea vizuri kadri iwezekanavyo pasipo vikwazo.

## 2.3 Kufanya Utafiti na Watoto Wakiwa Washiriki

Iligundulika mapema kwamba kuna changamoto maalum katika kupata data ya takwimu ambayo inaweza kulinganishwa katika maeneo tofauti ya utafiti kupitia utafiti shirikishi wa watoto. Timu ya watafiti ambayo tayari ina uzoefu wa tafiti za watoto walishirikiana kuandaa zana za utafiti kwa kuzingatia uwezo mdogo wa watoto kutoweza kushughulishwa kwa muda mrefu; kulikuwa na haja ya kufanya utafiti uwe wa kufurahisha kwa upande wao, kutengeneza 'mazingira salama' ambayo yatawasaidia katika kutoa maoni yao bila wasi wasi wa kuathibiwa na wale walio na madaraka shuleni au katika jamii zao.

Changamoto kubwa ilikuwa kwenye ubadilishaji kati ya msingi wa utafiti shirikishi ambao unaendeshwa kwa washiriki na mazingira yao, na hitaji la kiutendaji la kuweka kiwango kimoja kwenye zana za utafiti ili matokeo ya utafiti kutoka maeneo mbali mbali na maoni ya watoto wa umri tofauti yaweze kulinganishwa. Kwa ujumla, hili lilifanikiwa vizuri, lakini kuna maeneo katika ripoti hii (sura ya 3-5) ambayo waandishi hawakuweza kurejea maeneo yote kumi au vikundi vyote ishirini vya utafiti. Hii ni kwa sababu watafiti waliishiwa muda, na hasa kutokana na sababu kwamba kikundi husika kilitumia muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa katika mazoezi na michezo, au katika kuelewa swali linalohusika, au walikuwa wanachoka, au walihitaji kuachiwa waende nyumbani, hivyo watafiti walichukua maamuzi pale pale ya kuacha kuuliza swali fulani kwa kundi hilo.

Jambo lingine la muhimu ni maadili ya kufanya kazi na watoto. Hili lilichukuliwa katika sura tatu tofauti: kufanya mashauriano na watoto wakati wa kuandaa zana za utafiti, jitihada za kuhakikisha kuwa inapatikana ridhaa ya dhati ya watoto (na wazazi wao) kushiriki katika utafiti na kuhakikisha kuwa watoto hawakuhatarishwa kwa namna yoyote ile kutokana na ushiriki wao katika mradi wa utafiti.

Taarifa zaidi kuhusu zana za utafiti, jinsi zilivyotengenezwa na kutumiwa, na zana zilizotumika katika uchambuzi wa taarifa zipo katika kiambatisho 1.

## 2.4 Utayarishaji wa Ripoti Hii

Mada na masuala mbalimbali yalijitokeza wakati wa uchambuzi wa taarifa na katika kuandika ripoti hii; iliamuliwa ripoti ijikite katika masuala haya, kwa sababu yanaakisi vizuri zaidi maoni ya watoto. Mchakato wa kutengeneza zana za utafiti ulikuwa ni wa: kuzigawa mada kuu mbili katika vipengele vidogo vidogo ambavyo ni rahisi kueleweka kwa watoto; uandishi wa ripoti hii umekuwa ni mchakato wa kuunganisha vipengele vidogo vidogo katika mada yake kuu ili kutoa picha kamili, badala ya kuandika tu swali baada ya swali kuhusu waliyoyasema watoto.

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 8

# SURA 3 Vipengele Muhimu

## 3.1 Eneo la Kijiografia

Picha ya ujumla iliyokuwepo ni kwamba maeneo ya kijiografia (mijini, karibu na mijini au maeneo ya vijijini) yasingeleta tofauti kubwa kwenye maoni ambayo yangetolewa na watoto. Tofauti kubwa ingejitokeza kati ya Dar es Salaam na maeneo mengine nchini. Matokeo ya watafiti ni kwamba watoto wa Dar es Salaam walikuwa wepesi kuelewa dhana za habari, kama vile habari gani wanataka na kuzihitaji, na kama waliweza kuzipata wakati walipozihitaji. Pia walikuwa na fursa nzuri ya kuwa na vyanzo vingi vya habari, vikiwemo televisheni, simu za mkononi na matangazo. Watoto wa vijijini hutengemea sana mawasiliano ya ana kwa ana na mapokeo ya mdomo kutoka kwa wanafamilia na walimu, na wakati mwingine kwa njia ya simu.

Vijitabu vilivyotolewa kama shukrani kwa ushiriki wao kwenye utafiti, vilipokelewa kwa shukrani lakini hapakuwa na mshangao wowote kwa washiriki wa Dar es Salaam na Mwanza (yote ni maeneo ya mijini) na Tanga (karibu na mjini) ambako, watafiti wanahitimisha kwamba katika maeneo haya, kupokea au kumiliki kitabu ni kitu cha kawaida. Hii ni tofauti na baadhi ya maeneo ya vijijini, ambako watoto waliangalia tu vitabu na kisha kuwarudishia watafiti, hawakuamini kuwa ni zawadi ambazo wanaweza kubaki nazo.

Watoto wa Dar es Salaam pia walikuwa na malengo tofauti ya kazi za badaye - ambazo ni pamoja na kuwa malikia wa urembo na wachezaji wa mpira wa miguu/makocha.

## 3.2 Kipato cha Wazazi

Tatizo kubwa ambalo lilionyesha tofauti kati ya viwango mbalimbali vya kipato ni kwamba watoto wa maeneo yenye 'kipato kidogo' walizungumzia wajibu wao kama wanafunzi ni kuwa na bidii kama njia mojawapo ya kufannya vizuri katika elimu. Wanafunzi wa Dar es Salaam walitoa mifano kadhaa: kuwa wasikivu zaidi darasani, kutokutoroka shule, kusoma kwa bidii na kuwasikiliza wazazi na wakubwa. Watoto wa Tanga na Arusha hawakufafanua zaidi ya kusema tu 'kusoma kwa bidii'.

Katika vikundi ya viwango mbali mbali vya kipato, hakukuwa na tofauti kubwa kuhusu kazi za baadaye ambazo watoto walizitamani, lakini inaonekana kuwa watoto wanaotoka katika familia maskini wameshajua kuwa kupata elimu bora haitakuwa rahisi.

## 3.3 Umri wa Washiriki wa Ufatifi

Kulikuwa na mwelekeo wa watoto wakubwa kuwa na uelewa mzuri wa dhana na ufahamu mpana wa masuala husika. Walipoulizwa kuhusu kazi za baadaye walizotamani, watoto wadogo walikuwa na maoni kidogo kuhusu kazi ambazo wangependa kuzifanya ukilinganisha na watoto wakubwa[13].

Watoto wadogo walitoa jumla ya mapendekezo 26 ya jinsi ya kuboresha elimu, wakati watoto wakubwa waliainisha njia 40, na mapendekezo yao mara nyingi yalikuwa mazuri na yenye malengo maalum. Watoto wakubwa wa Dar es Salaam, kwa mfano, walitaja haja ya kuwa na mafunzo kwa vitendo ili kuwasaidia katika elimu yao: *“tunasikia tu ukichanganya asidi na besi unapata chumvi na maji, lakini hatujapata kuona kwa macho yetu wenyewe”,* badala ya *“kufundishwa vizuri tu”* - ambako kulitajwa na watoto wadogo wa Arusha, Tanga na Mwanza, pamoja na baadhi watoto wakubwa wa Singida.

Awali watoto wadogo wa Terat (Arusha) walipata wakati mgumu kutofautisha mkono wa kushoto na wa kulia, japokuwa baada ya mazoezi kidogo ya pasha joto ilionyesha kuwa kiwango chao cha Kiswahili kinatosha katika kukidhi mahitaji ya utafiti.

13 Watoto wadogo walikuwa na wastani wa mapendekezo 7.7, wakati vikundi vya watoto wakubwa walikuwa na wastani wa 9.2

## 3.4 Jinsia

Methodolojia yetu ililenga kuwa na ushiriki mpana wa vikundi na hakukuwa na tofauti kati ya utayari wa wasichana na wavulana walioshiriki kutoa mawazo yao kwa uwazi. Tofauti za kijinsia hazikuwa wazi katika mambo mengi waliyowaambia watafiti, yakiwemo, kwa mfano katika mgawanyo wa kazi za nyumbani ambako tofauti kubwa kijinsia ilitarajiwa. Kinyume chake, kulikuwa na malalamiko kwa kikundi kimoja cha mjini kwamba baadhi ya wavulana hawakufanya sehemu ya kutosha ya kazi, jambo ambalo linaashiria kuwa kulipaswa kuwa na mgawanyo sawa wa kazi.

Tofauti kubwa za kijinsia zilizojionyesha zilitokana na kazi za baadaye ambazo watoto walitamani kuzifanya. Tofauti za kawaida za mgawanyo wa kazi kijinsia zilionekana ikiwa ni 89% ya wasichana wanaotamani kuwa manesi, na 70% ya wale wanaotaka kuwa walimu. Kwa upande mwingine, zaidi ya theluthi moja ya wale wanaotamani kuwa marais pia walikuwa ni wasichana, na karibu nusu ya wanaotamani kuwa marubani ni wasichana. Taarifa za kina za malengo ya kazi zimeelezwa katika sehemu 5.4.

Ushahidi mwingine pekee wa tofauti za kijinsia ni kwenye ripoti za watoto kuhusu tofauti kati ya wazazi. Walisema mama wanasikiliza watoto zaidi kuliko baba kwa masuala kama ya mahitaji ya shule na mahitaji ya nguo, lakini tofauti hizi haziko wazi na siyo za uhakika. Katika baadhi ya jamii akina baba walikuwa wakielezwa tu masuala yanayohusiana na kusoma.

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 11

# SURA 4 Maoni ya Watoto kuhusu Shule, Ufundishaji na Kujifunza

Mojawapo ya mambo yaliyobainika kwenye matokeo ya utafiti ni kwamba wakati watafiti walikuwa wametengenisha katika makundi mawili zana za utafiti, moja ikihusisha kusoma shule na nyingine ikiwa ni nafasi ya watoto katika jamii, tofauti hiyo haikuonekana katika majibu ya watoto. Kwao, mambo haya mawili yameunganika na huingiliana sana. Wanafamilia na walimu ni vyanzo vikuu vya habari ambazo watoto huzitumia kujifunza mambo muhimu katika dunia pana. Wataalamu wa sekta ya elimu wanaweza kusisitiza walimu, vitabu na miundombinu kama vipengele muhimu vya elimu, lakini mtazamo wa watoto ni wa ujumla zaidi ukiangalia pia kujifunza kutoka kwa wazazi, na miongoni mwao wenyewe, na kujali mazingira ya shule kwa ujumla, yakiwemo masuala kama ya upandaji miti.

Kwa upande mwingine, kuna tofauti inayoshangaza katika majibu ya watoto. Kwa mfano, hawajataja hata mara moja faini - kama aina ya adhabu, zinazotokana na kuharibu mali za shule au vitabu, lakini faini zilitajwa mara nyingi kama mchango kwa shule. Sababu ya hali hii siyo dhahiri - inawezekana wazazi hulipa faini na mtoto haelewi tofauti kati ya faini kwa uharibifu na mchango mwingine wa kawaida?

Vile vile, kuchapa kulitajwa na 90% ya shule kama sifa mojawapo ya mwalimu mbaya, lakini kulitajwa na 60% wakati wa mijadala kama adhabu. Labda watoto wanaona kuwa kiasi fulani cha kuchapa kama sehemu ya kawaida ya kufundisha/kujifunza na siyo lazima iwe ni adhabu? Hakika kunahitajika utafiti zaidi kujua tofauti hizi katika mitazamo.

## 4.1 Huduma Shuleni

Uulizaji wa maswali kuhusu mlolongo wa huduma zinazotolewa shuleni na uzuri wake ulitokana na mazungumzo na watoto wakati wa mchakato wa kuandaa zana za utafiti. Ilionekana kwamba kwa wale watoto shule ni zaidi ya vyumba vya madasa, walimu na vitabu. Watoto walisema kuwa suala la mazingira, afya, maji safi na salama na chakula ni muhimu pia kuzingatiwa.

**Mazingira**

*'Maeneo ambayo yanatuzunguka tunapoishi na kusoma'* (Tanga). Hata watoto wadogo kabisa waliweza kuelezea vipengele vya mazingira mazuri, japokuwa wadogo wengi walijikita zaidi kwenye misemo kama vile *'mazingira ni rafiki'* (Arusha). Kwa watoto mazingira hayakumaanisha tu miti na majani katika maeneo ya shule, lakini pia mazingira ya shule, hali ya madarasa na madawati, na kama yanatosha pamoja na usafi wa ujumla - hasa wakimaanisha ufagiaji. Vikundi kadhaa pia walitaja uwepo wa ofisi ya walimu kama sehemu ya mazingira mazuri. Watoto wa Lindi walitaja mahususi kwamba wana watoto 120 kwenye darasa moja na haya ni mazingira mabaya.

**Afya**

Majibu ya watoto kuhusu upatikanaji wa huduma za afya shuleni yalionyesha kuwa walijua fika umuhimu wa lishe bora na wa shule kutoa chakula kwa wanafunzi pamoja na upatikanaji wa maji safi kama vipengele vya afya zao. Kuna mkanganyiko kwamba watoto hufundishwa kuhusu masuala haya kama sehemu ya mtaala, lakini shule zenyewe hazina uwezo wa kutimiza mahitaji haya ya kimwili ya wanafunzi.

Majibu mengi ya wanafunzi kuhusu huduma za afya shuleni yalihusiana na uwepo wa sanduku la huduma ya kwanza, au urahisi wa kupata ruhusa ya kwenda hospitali, na umbali wake. Nusu ya shule zilizokuwa kwenye sampuli, zilikuwa na aina fulani ya huduma ya kwanza. Katika shule nyingine, mtoto mgonjwa hupelekwa kituo cha afya au hospitali iliyopo karibu. Dar es Salaam ina hudumu nzuri zaidi za afya, watoto wakiripoti kupata chanjo wakiwa shuleni, huduma za matibabu ya meno na kupewa dawa ya mswaki. Shule moja ilihakikisha kuwa watoto wa darasa la kwanza wanapata matibabu bila kulipia, na katika shule nyingine, watoto wakubwa walikumbuka kuwa wakati fulani siku za nyuma ukienda na daftari la wagonjwa unaweza kupata huduma za afya bure, lakini sasa hivi unatakiwa kulipa Tshs. 1,000/. Shule moja tu haikuwa na utaratibu wa huduma za afya kwa watoto wagonjwa.

**Maji**

Kwa mara nyingine tena, watoto wanajua fika umuhimu wa maji safi, kwa kufulia/kuogea na kwa ajili ya kunywa. Umuhimu wake unakuwa mkubwa zaidi pale ambapo watoto wanatembea umbali mrefu kwenda shule na hivyo kupata kiu. Hata hivyo ni shule mbili tu zilizokuwa kwenye sampuli (Mwanza na Tanga) zilikuwa na maji ya kunywa ya bomba kwa ajili ya watoto. Kwa Dar es Salaam, watoto ama walileta maji kutoka nyumbani au walinunua kwenye maduka yaliyo karibu na shule.

Kaimu Mwalimu Mkuu wa shule moja alitaja kipindupindu na kuharisha kama matatizo yanayotokea shuleni mara kwa mara kwa sababu ya matatizo ya maji. Watoto katika shule hiyo walithibitisha kuwa hupata maji ya kunywa wakati wa mchana kama tu wakirudi nyumbani wakati wa mapumziko. Watoto 10 kati ya 25 kwenye sampuli ya watoto wadogo zaidi husubiri mpaka mwisho wa siku wanaporudi nyumbani ndipo hupata maji ya kunywa yaliyochemshwa.

**Chakula**

Shule tatu tu (30%) kati ya zile zilizokuwa kwenye sampuli hutoa chakula kwa watoto kila siku; moja ikiwa ni ya wenye kipato cha juu na mbili za kipato cha wastani - na hata kwa hizi shule mbili mpango huu unaonekana kutokufuatwa kwa sasa. Katika shule nyingine mbili (Arusha na Dar es Salaam) ilionekana kwamba chakula cha kuuzwa hupatikana kwenye maduka madogo yaliyopo karibu na eneo la shule. Shule nyingine moja ina shule ya awali na hutoa huduma ya uji kwa wanafunzi kwa gharama Tsha 1,500/- kwa mwezi.

Watoto wa Mtwara walisema kuwa mwaka uliopita walipata mahindi kidogo, viazi na maembe kutoka kwenye shamba la shule; wakati katika maeneo mengine kufanya kazi katika shamba la shule kulitajwa kuwa ni mchango wanaoutoa watoto kwa shule, hawakutaja faida zake kwao, kama vile kula wanachokizalisha.

Kwa kuwa kuwapa watoto chakula shuleni kunaboresha mahudhurio yao, na pia huongeza uwezo wao wa kujifunza na kwa kuzingatia umbali mrefu ambao watoto hutembea kwenda shuleni[14], inaonekana jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha mahitaji ya lishe kwa watoto yanatimizwa.

## 4.2 Vitabu

Watoto walioshirikishwa wakati wa kubuni utafiti huu waliainisha suala hili kama kipaumbele. Kwa ujumla suala la vitabu vya kiada linaeleweka vizuri: karibu 80% walisema wanavielewa vitabu vyao vya kiada, lakini vitabu ni vichache. Sehemu ndogo ya sampuli - 15% walisema wana vitabu vya kutosha. Matokeo hayaonyeshi tofauti yoyote kwa umri wa watoto, kiwango cha kipato au tofauti za kijiografia.

Idadi ya vitabu na urahisi wa kuvielewa, ni masuala yanayohusiana. Mtoto mmoja mdogo alisema kuwa vitabu vitakuwa rahisi kuvielewa kama watu wanaoshirikiana kitabu kimoja hawazidi watatu. Watoto wakubwa katika shule moja walisema kitabu kimoja kinatumiwa na wanafunzi mpaka 20 - jambo ambalo halikupingwa kwenye mkutano na walimu wao - na kusema kwamba vitabu vitakuwa rahisi kuvielewa kama kurasa hazijachanwa au kunyofolewa. Kitabu ambacho kinapita kila dawati mara kwa mara na kutumiwa na wengi ni rahisi kuchakaa.

Kwa kweli walimu wana wakati mugumu sana katika kuwaruhusu watoto kutumia vitabu kwa muda wao wenyewe. Kwa kawaida vitabu hukusanywa mwisho wa kila kipindi. Mtoto mmoja alionyesha kuridhishwa kwamba mwaka huu wameruhusiwa kwenda nyumbani na vitabu, lakini katika shule nyingine vitabu havitolewi tena kwa sababu mwaka uliopita vilipotolewa baadhi havikurudishwa. Shule nyingine huwatoza faini wanafunzi wanaopoteza vitabu, na kwa shule moja wanafunzi wote walipaswa kuchangia pale ambapo mwenzao mmoja amepoteza kitabu. Baadhi ya watoto walilalamika kuwa

14 National Bureau of Statiscts (2007) The 2007 Household Budget Survey, Community Characteristics, inaeleza muda wanaotumia wanafunzi wa shule za msingi kwenda shule. Walio umbali wa zaidi ya saa moja kutoka shule ya msingi ya serikali iliyo karibu ni 3.2% (ukurasa 9) lakini kwenye baadhi ya maeneo ya vijijini hii inaweza kuwa mbali zaidi ya saa moja.

vitabu havigawanywi kwa usawa katika madarasa yote, kwa mtazamo kwamba - katika shule moja - darasa la 4A hupata vitabu vingi zaidi kuliko 4B au C, lakini watafiti walishindwa kuhakikisha hili kupitia vyanzo vingine.

Watoto pia walitoa ushauri mzuri. Aina ya vitabu wanavyovitaka viwe na maumbo makubwa (hii ni kutoka kwa mtoto mkubwa), na picha ziwe na uhalisia au zihusu hali wanayoweza kuielewa.

## 4.3 Walimu

Watoto waliongea sana na kwa undani walipoelezea sifa za walimu wanaowaelewa - *wanaeleweka* na wasiowaelewa - *wasioeleweka* (walimu wabaya). Kwa sababu ya unyeti wa suala hili na uelewa wa watafiti kuhusu changamoto zinazowakabili walimu katika shule nyingi, watafiti walikuwa makini kutoa fursa kwa watoto kuzungumzia sifa zote nzuri na mbaya, na kwa kweli majibu ya watoto yalikuwa kwenye uwiano mzuri wakielezea wanachokipenda na wasichokipenda.

Kuna baadhi ya matokeo ya utafiti ambayo ni mabaya, na katika kuchambua matokeo watafiti walikuwa makini kuepuka kutoa tafsiri isiyo sahihi. Kwa mfano, (wa kubuni tu) watoto wangesema kuwa mwalimu mbaya ni yule anayewapa watoto sumu, hiyo inamaanisha lazima kuna mwalimu anayewapa sumu shuleni kwao? Bila kuwa na muda na rasilimali za kutosha kuchambua vizuri wanachokisema watoto watafiti wasigeweza kuwa na uhakika. Hata hivyo ni rahisi kuona kuwa katika shule moja ambapo hakuna ripoti za utoro wa walimu, watoto hawakutaja mahudhurio mazuri kama sifa ya mwalimu mzuri - kwamba anahudhuria vipindi, au kutokuhudhuria kama sifa ya mwalimu mbaya - kwamba hawahudhurii; - inaonekana kuwa mahudhurio ya walimu yalichukuliwa ni kitu cha kawaida. Katika maeneo mengine yote ya utafiti walitaja bayana kuwa mahudhurio ni suala la kuzingatia; kwa hiyo, sifa ya mwalimu mzuri au mbaya ilihusisha iwapo mwalimu alihudhuria kipindi na kwamba alifundisha kweli. Kutokana na hili ni haki kuhitimisha kwamba watoto wanapotaja sifa mbaya wameona mfano wake.

Wakati mwingine majibu waliyotoa watoto yalikuwa tofauti. Mwalimu mzuri anasahihisha madaftari, na mwalimu mbaya ni yule anayetoa kazi halafu hasahihishi. Hata hivyo, kwa kuangalia maelezo ya jumla ya watoto, mambo matatu yametajwa katika walau shule 9 kati ya 10:

1. Mwalimu mzuri ni yule anayefundisha mpaka wanafunzi wanaelewa, anayeendelea kuwafundisha hata pale ambapo hawaelewi na huwapa msaada wa ziada na ana bidii.

2. Walimu kushindwa kuhudhuria kwenye vipindi na kufundisha ni suala lililotajwa na 90% ya shule zilizotembelewa

3. Adhabu ya viboko, au hofu yake, ni tatizo kwa 90% ya wanafunzi katika sampuli. Nidhamu inajadiliwa katika sehemu inayofuata, itoshe tu kusema kuwa tatizo hasa siyo kuchapa bali hofu ya kuchapwa. Katika shule tatu ilitajwa kuwa mwalimu anayeingia darasani akiwa na fimbo huwaogopesha watoto au watoto wanaanza kutetemeka.

Ni muhimu kusema tena kwamba msisitizo wa zana za utafiti ulikuwa ni kwa walimu ambao wanafunzi wanawaelewa na wale wasiowaelewa. kinachoonekana ni kwamba watoto wanasema hawawezi kumwelewa mwalimu, yaani kujifunza kutoka kwake katika muktadha wa woga na kwamba kutembea tu na fimbo kunaleta woga.

Maoni ya jumla ya watoto kuhusu walimu wazuri na wabaya, yanaweza kuchambuliwa katika makundi yafuatayo:

1. Maoni wanayoyatoa watoto kuhusu wanachokitaka kutoka kwa walimu, yanaonyesha ufahamu wa masuala kama vile mawasiliano kati ya shule na familia, na ufahamu wa jinsi kila mwalimu anavyoonekana katika jamii nzima.

2. Mapungufu, kwa maana ya mambo ambayo watoto wanayapata kutoka kwa walimu wao:

   (i) Kushindwa kutimiza wajibu wa kimkataba, kwa maneno mengine kutokufanya kazi wanayolipwa kuifanya kwa kiwango chake

   (ii) Kushindwa kufuata maadili mazuri ya elimu, kwa maneno mengine walimu wanakuwepo darasani lakini hawatimizi wajibu wao kwa njia ambayo itasaidia kulete ufanisi katika kujifunza.

3. Hali ya ujumla ambayo haiwataji sana walimu kama wawezeshaji wa kujifunza, methodolojia shirikishi ya kujifunza/kufundisha.

Wakati mwingine baadhi ya maoni ya wanafunzi huwaonyesha walimu katika hali ya ubaya sana, watafiti pia waliona mifano ya vitu vizuri, kuchukua hatua za kutoa maji safi ya kunywa na kufanya juhudi za kuwawezesha watoto wenye matatizo ya kuona kuwa sehemu ya shule.

**Wanachokitaka Wanafunzi Kutoka kwa Mwalimu**

Mtazamo mkubwa na usioshangaza ni kwamba mwalimu ni mtu anayefundisha mpaka watoto waelewe, na anayekupa msaada unapokuwa huelewi. Watoto walifikiri ni muhimu kwa mtu huyo kupenda kufundisha na kuwapenda wanafunzi. Wanataka mtu huyo awe na bidii na achangamke na wanafunzi, anayeweza kucheka na wanafunzi na kwa mujibu wa kikundi kimoja ashiriki michezo.

Mwalimu mzuri ni mtu anayetoa mifano mizuri, na zaidi ya mfano mmoja, anaongea pole pole, na katika shule moja walitaja kabisa aongee Kiswahili - pengine kwa sababu ndiyo lugha ambayo wanaielwa kwa urahisi. Mwandiko unaosomeka ubaoni ulitajwa kuwa ni muhimu katika shule tatu kati ya kumi.

Kuhusisha walimu wazuri na wabaya na kufaulu mitihani kulitajwa mara moja na watoto katika utafiti wote.

Maoni yalitolewa kuonyesha kwamba watoto wanahitaji kitu zaidi kutoka kwa walimu wao zaidi ya kusoma tu. Watoto walitaja mara nyingi kwamba mwalimu mzuri huwauliza wanafunzi maswali, lakini hii haikueleweka vizuri iwapo hii inahusiana na mwalimu kutaka kujua kama watoto wameelewa mada husika, au kwa ujumla kupenda kujua kwa upana ustawi wa watoto. Kulikuwa na viashiria kuwa watoto walihitaji sehemu ya yote haya kutoka kwa walimu, huku kundi moja la watoto likisema kuwa mwalimu mzuri huwashauri watoto, na lingine likisema mwalimu mzuri ni yule anayewashirikisha watoto na kusikiliza majibu wanayotoa watoto.

Watoto pia wanaelewa masuala mapana kuhusu uhusiano wao na wazazi na jamii nzima. Hawakuwapenda walimu ambao matendo yao siyo safi katika jamii na walidhani kuwa mwalimu mzuri hufuatilia maendeleo ya watoto na anawaeleza wazazi. Kinyume chake, walimu wabaya huwakatisha tamaa wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto. *'Wazazi wanapotaka kujua maendeleo ya wanafunzi huwakoromea'.*

**Kushindwa Kutimiza Wajibu wa Kimkataba**

Katika kila shule isipokuwa moja tu wanafunzi walitaja matatizo ya walimu kutokuhudhuria darasani, au kwenda darasani lakini hawafundishi, kuingia kisha kutoka tena, anakuja wiki moja kisha wiki inayofuata anaacha kabisa, anatoka kabla kipindi hakijaisha, anaruka mada zingine au anasinzia tu darasani. Katika shule moja wanafunzi walizungumzia madhara ya kutokuwa na walimu wa kutosha, na baadhi ya madarasa yalikosa walimu wa kuwafundisha na wakati mwingine mwalimu anaumwa lakini analazimika kuingia darasani. Hata hivyo, hali ya ujumla ni kwamba kiwango kikubwa cha wanafunzi wamekatishwa tamaa na walimu kutokutimiza wajibu wao ambao wanalipwa kuutekeleza.

Kwa shule zingine hali ni mbaya zaidi, huku wanafunzi wote wakubwa kwa wadogo wakisema kuwa mwalimu mbaya ni yule anayekunywa pombe wakati akiwa darasani anafundisha, kwa shule nyingine mwalimu mbaya ni yule anayevuta bangi, na kwa shule nyingine ni wale wanaokula rushwa.

Ukweli kwamba mwalimu anaingia darasani na fimbo, na mitazamo ya watoto ikiwa ni kwamba inaweza kutumika, inaonyesha kwamba taratibu za serikali kuhusu adhabu ya viboko hazifuatwi. Vile vile, wanafunzi katika shule moja ya watu wenye kipato cha chini walilalamika walimu kuwatoza hela ya masomo ya ziada na kufundisha madarasa hayo ya ziada muda kabla ya vipindi ambavyo wote wanatakiwa kushiriki. Hii inaashiria kwamba kama siyo uvunjaji mkubwa wa kanuni basi walau ni kinyume na maadili na kutokuwajali wanafunzi maskini.

**Kiwango Kibaya cha Weledi**

Watoto walitoa mifano mingi ya vitu ambavyo hawavipenda kwa walimu, picha ya ujumla ikiwa ni kwamba shule 9 kati ya 10 kuna walimu ambao hawapendi kufundisha, au hawapendi wanafunzi na/au ambao wana hasira au ni wavivu. Watoto walitaja mahususi mambo yafuatayo kuwa hawayapendi:

1. Walimu wakali, wanaofundisha kwa hasira, wakipaza sauti na kutumia lugha chafu pamoja na adhabu za viboko.

2. Walimu wanaowapa mazoezi na kuwataka waandike kwenye madaftari kisha hawasahihishi au husahihisha baada ya muda mrefu kupita.

3. Walimu wanaowanyanyasa wanafunzi

4. Kumwambia mwanafunzi mmoja aandike ubaoni na wengine wanakili tu bila yeye kuelezea chochote.

5. Walimu wanaoanza kuuliza tu maswali pasipo yeye kwanza kuelezea chochote, au walimu wanaoingia darasani wanagawa vitabu na kutoa kazi bila kuelewesha kisha huwachapa watoto wakikosea kujibu maswali.

6. Mwalimu anayewaambia waende wakawaulize wanafunzi wa madarasa ya juu ikiwa hawaelewi.

7. Mwalimu anayeleta utani mwingi kisha kuondoka bila kufundisha.

8. Walimu wanaoongea haraka haraka, hasa kwa Kiingereza

9. Walimu wenye sifa mbaya kwenye jamii.

Wakati mwingine wanafunzi waliwalaumu pia walimu kwa vitu ambavyo siyo lazima iwe ni makosa yao, lawama kama za kugawa vitabu mwanzo wa kipindi na kuvikusanya baada ya hapo. Walimu wanaweza kuwa wanafanya hivi ili kuhakikisha vitabu vinadumu kwa ajili ya miaka inayofuata. Kadhalika, picha inayojengeka ni kuwa wanafunzi wamekata tamaa katika kukidhi kiu yao ya kujifunza.

**Taswira Pana Zaidi**

Zaidi ya kurekodi tu maoni ya watoto kuhusu walimu wao, kuna nafasi ya kwenda ndani zaidi kuchunguza kilichosemwa na kisichosemwa. Kwa mfano, kufaulu mitihani kulitajwa mara moja tu wakati wote wa majadiliano. Pengine kwa wanafunzi hilo lilikuwa suala la lazima ambalo halihitaji hata kutajwa, lakini mara nyingi waliainisha masuala yaliyoashiria kuwa walipenda mahusiano: yaani, walimu wanaowapenda na kujitahidi, wanaosikiliza majibu ya wanafunzi na wanaowasiliana na wazazi wao, tofauti na walimu wanaoonekana wana hasira sana au wakali au wasiowajali kiasi kwamba hukosa viwango vya msingi vya weledi.

Inafurahisha kuona kwamba nia ya watoto katika mawasiliano kati ya wazazi na wanafamilia na walimu inaendana na utafiti wa kimataifa unaohusu kuboresha matokeo ya elimu. Wakati njia za kufanya hivi zipo, kwa mfano kamati za shule, inaonekana, kama itakavyoripotiwa baadaye (sehemu 5.3), kwamba hakuna jukwaa zuri linaloweza kuwaleta pamoja wahusika wote (walimu, wazazi na wanafunzi) ili kujadili mahitaji na vipaumbele. Mkoani Tanga pekee watafiti waliona ushahidi wa kamati ya wazazi ikiwasiliana

kikamilifu na walimu kuelezea wasiwasi wao wenyewe na wa watoto. Hakuna bajeti kwa ajili ya ripoti ya shule kwa shule za msingi - shule nyingi zinaitisha siku ya wazazi; lakini hii siyo fursa ya kujadili maendeleo ya mwanafunzi mmoja mmoja.

Walimu katika baadhi ya shule zilizotafitiwa hawakukubaliana na nia ya watafiti ya kuomba ruhusa ya wazazi ili kuzungumza na watoto wakati wa utafiti. Kwa maoni yao hakukuwa na haja ya kuomba hiyo ruhusa kwani utafiti utafanyika wakati wa shule, ilikuwa tu ni kwa walimu kuamua kitu gani watoto wakifanye wakati wa saa za shule. Inawezekana ni kutokana na mtazamo huo ndio maana walimu wanawafanyisha wanafunzi kazi za ndani katika nyumba za walimu.

Katika muktadha wa mitazamo na mahusiano ya aina hii, inaonekana kuwa mbinu shirikishi za ufundishaji hazitaweza kuanza kutumika siku za karibuni. Mwalimu mzuri ambaye anaonekana ni yule anayewafundisha watoto mpaka waelewe inaashiria ni lazima awe na ujuzi mzuri wa kujua seti fulani ya maarifa badala ya mwalimu anayewasaidia watoto kuilewea dunia pana na kuwawezesha kupata stadi za kushiriki katika dunia hiyo. Katika shule tatu kati ya kumi msisitizo ulikuwa wa walimu kuwa na mwandiko mzuri ubaoni unaashiria kuwa kunakili maandishi kutoka ubaoni ni shughuli muhimu - na kwa kweli ni mbinu muafaka ya kuwaweka kimya watoto wengi darasani na kuwa na shughuli ya kufanya. Kwa bahati mbaya hii hufanyika pasipo ushirikishi wa kutosha wa haya yanayonakiliwa, na kama wanafunzi wakati mwingine walivyolalamikia, zoezi hili wakati mwingine haliambatani na mwalimu kutoa maelezo. Inashangaza, kikundi kimoja cha watoto wadogo (Mwanza) walisema kuwa mwalimu mbaya anawafundisha watoto kufikiria. Mtazamo wa aina hii, ukiwekwa pamoja na ukosefu wa mbao za matangazo kuwajulisha watu shughuli za shule, na watoto kutokujua masuala yanayojadiliwa katika kamati zao za shule, ukosefu wa uwakilishi wao kwenye kamati hizo (yote yameelezwa katika sehemu inayofuata), yanatoa taswira pana zaidi ya mtazamo finyu wa kusoma. Inaonekana watoto wengi wameshachukua mtazamo huu finyu, ambao una nafasi ndogo sana ya kusaidia maendeleo ya watoto na kuwaelimisha kikamilifu na kuwapa stadi za kuchukua nafasi yao na kutimiza wajibu wao katika jamii.

## 4.4 Nidhamu na Adhabu

Mtazamo huu unatokana na nafasi kubwa inayochukuliwa na adhabu katika maisha ya watoto shuleni. Kama ilivyotajwa kabla, hili ni moja ya mambo matatu yaliyoibuliwa na watoto kuelezea ufundiashaji wanaoweza kuuelewa au wasioweza kuuelewa. Ili kutokuharibu mjadala unaohusu 'hadithi za kutisha' kuhusu matumizi mabaya ya adhabu ya viboko, watoto waliulizwa unafanywaje ukifanya jambo sahihi. Wengi walijibu kuwa hupata zawadi kutoka kwa walimu, kama vile vitabu, kalamu au hata sokisi na viatu. Hakuna aliyetaja kuwa atafaulu mitihani, kupata alama nzuri, ripoti nzuri kutoka kwa mwalimu kwenda kwa wazazi au mguso wowote wa ndani wa kujua kitu ambacho alikuwa hakijui kabla.

Shule siyo mahali pekee ambapo watoto wanaadhibiwa. Nyumbani huchapwa kama wasipokwenda shule. Watoto wa Mtwara walitaja adhabu mbili za nyumbani wasizozipenda, kunyimwa chakula na kufukuzwa nyumbani ili kwenda kulala porini. Hii inaweza kuwa sababu ya kukataa kusaidia kazi za nyumbani kama kuteka maji au kusaidia shambani. Hivyo, siyo sahihi kuona nyumba zote ni mahali ambapo watoto wanasikilizwa na kulelewa, kama ambavyo shule siyo sehemu pekee ya unyanyasaji.

Siyo nyumbani wala shuleni dhana ya kufanya makosa haijadiliwi. Haikutajwa kuwa ni mazingira yanayoweza kumfanya mtoto asikilizwe na walimu au wazazi. Hoja moja iliyotolewa ya mwalimu mzuri ni yule ambaye anaelewa kama ukichelewa - hii ilitoka shule moja ya Rukwa ambako baadhi ya watoto wanakaa mbali sana na shule.

Watoto walipoulizwa kuhusu sifa za mwalimu mbaya au yule ambaye hawamwelewi, kuchapa viboko kulitajwa katika shule tisa kati ya kumi. Hata hivyo walipoulizwa hususan kuhusu adhabu, kuchapwa kulitajwa na vikundi kumi na moja kati ya vikundi kumi na tisa, kama sehemu ya adhabu nyingine nyingi ambazo zitajadiliwa baadaye. Maelezo ya hili hayapo wazi, lakini inawezekana ni kwa sababu watoto kwa kiasi kikubwa wanakubali kuwepo kwa adhabu, wanailalamikia pale tu adhabu inapokuwa ya kionevu. Hasa, watoto wenyewe walitofautisha kuchapwa kwa kukosa na kuchapwa bila sababu, au

kwa sababu adhabu haiendani na makosa aliyoyafanya mtoto.

Kanuni za taifa za adhabu ya viboko zinatoa taratibu za nani anaruhusiwa kutoa adhabu hiyo - Mwalimu Mkuu au mwalimu ambaye amekasimishwa kutoa adhabu hiyo akitumia fimbo laini na kuchapa mikononi tu. Inaonekana kwamba kanuni hizi hazifuatwi maeneo mengi. Kama ingekuwa inafuatwa watoto wasingeogopa kwa mwalimu kuingia darasani na fimbo - kwa hakika wanaelewa kuwa fimbo hiyo haitumiki, mathalani, kuonyesha maandishi ubaoni. Watafiti pia waliwaona walimu wakitembea katika maeneo ya shule huku wameshika fimbo, jambo ambalo linadhihirisha siyo tu mwalimu wa nidhamu ndiye anatembea na fimbo au kutoa adhabu hiyo. Watoto wa shule moja (Dar es Salaam) walisema kuwa ukifanya kosa unachapwa na walimu wote[15]. Kwa mara nyingine tena watoto katika shule mbili za mjini walisema *'kupigwa mangumi'* na shule zingine mbili *'kuchapwa mikono',* katika shule nyingine *'kupigwa manjingo na makofi'* na pia *'kupigwa mabao ya masikioni'* - adhabu hizi kali zinazoumiza ziko nje kabisa ya kanuni za adhabu.

Watoto katika shule moja walisema walimu hawataki kuchapa mikononi badala yake wanataka wachape matakoni. Pale ambapo kanuni zinafuatwa, walau katika eneo hili, kwa shule ya Arusha watoto huchapwa viboko viwili tu mkononi adhabu ambayo watoto walisema inafaa kwa kuwa siyo kali.

Watoto waliripoti adhabu nyingi ambazo hata hazikutajwa kwenye kanuni za adhabu za viboko. Zipo katika vikundi yafuatayo:

1. Zile ambazo zinaumiza mwili (kupigwa makofi ya masikioni), na zinaweza kusababisha madhara ya muda mrefu. “Kushika masikio” kulitajwa na 70% ya shule. Watoto katika shule moja walitaja kabisa kuwa hii ni adhabu kali sana.

2. Mazoezi ambayo yanachosha mwili, lakini siyo lazima yalete maumivu makali. Hizi ni pamoja na aina zote za mazoezi, kuamzia kichura, push-ups, kupia magoti au kupiga magoti mikoni ikiwa juu au pembeni ni ya kawaida mno.

3. Zile ambazo hazipendezi, zinaudhi au zinatumia muda mrefu, lakini siyo ngumu au hatari; kama vile kufagia darasa, kusafisha vyoo au kuokota uchafu.

4. Shughuli ambazo zinatumia nguvu nyingi, hizi mara nyingi huhusishwa na kilimo, kama vile kulima, kupanda, kupalilia. Pia kuna kuchimba mashimo ya taka kwa ajili ya shule, kitu ambacho ni cha lazima kwa shule kuwa nacho.

Swali linalotakiwa kupata jibu kuhusu adhabu za aina hii ni kwamba: yanatarajiwa kuleta matokeo gani, na je inawezekana kuna matokeo mabaya yasiyotakiwa kutokana na adhabu hizi? Kama ilivyotajwa kabla hakukuwa na dalili yoyote ya mjadala wa makosa yanayofanyika kwa lengo la kurekebisha tabia za mtoto. Wakati mwingine kuna hatari ya kupata matokeo ambayo ni kinyume kabisa. Kwa mfano, wavulana katika shule mbili walisema kuwa ahabu kama kuruka kichura na push-ups siyo kali kwa sababu hufanya mazoezi ya aina hiyo ili kujiweka katika hali nzuri kiafya - hivyo inaonekana kitu ambacho wavulana hupenda kikifanya kwa kawaida kinatumika kuwaadhibu wao, hivyo hawatachukulia adhabu kama kitu cha msingi. Kwa upande mwingine kuna hatari ya kweli kuwa kazi kama kuweka mazingira ya shule katika hali ya usafi, au kufanya shughuli za kilimo ikitumiwa kama adhabu, kuwafanya watoto kuona kazi hizo ni nzuri au zina manufaa kama sehemu ya mtaala 'elimu ya kujitegemea' itakuwa ni shughuli ngumu sana kwa kuwa shughuli hizi tayari zinaonekana ni za wale wanaofanya makosa.

Haieleweki kama hali inakuwa nzuri au inakuwa mbaya. Hii haishangazi kwa sababu tofauti na idadi ya vifaa vya shule, hali kwa ujumla siyo rahisi kuiboresha mwaka hata mwaka labda kuwe kuna maagizo yanayokuja na kutekelezwa ipasavyo ili kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa au kuzibadilisha. Yote haya hayataweza kuwa na ufanisi bila kuwa na msukumo wa kutosha wa kuinua ari ya walimu na maslahi yao, na kuwapa mafunzo ya adhabu mbadala kwa viboko, kama mambo ya kuanzia.

[15] Watoto walieleza kwamba hali ya kawaida katika shule yao ni kumpeleka mwanafunzi mkosaji katika ofisi ya walimu ili achapwe, na walimu wote huja kila mmoja akisema kosa analolijua na kumchapa mtoto kwa makosa yote mapya yatakayosemwa na walimu hao.

## 4.5 Michango

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ulikuja na kanuni kwamba mtoto asikose elimu kwa sababu ya kushindwa kulipa ada, na ulitoa mchango mkubwa wa kujenga shule na kuweka 'mfuko maalum' kwa ajili ya gharama za uendeshaji zisizo mishahara, ili ada isiwe jambo la lazima. Utafiti huu unakusanya maoni ya watoto kuhusu kinachotokea katika mazingia yao.

Taswira inayojitokeza inatofautiana, japokuwa kuna aina fulani ya michango iliyotajwa na vikundi 19 kati ya 20. Hakuna mwelekeo mahususi kuhusu viwango vya kipato au hali ya kijiografia. Vikundi vya watoto wadogo na wakubwa katika shule moja havikueleza gharama zinazofanana na viwango vinavyofanana vya michango. Neno 'ada' lilitajwa na kikundi kimoja tu, japokuwa kuna aina tofauti za michango huku baadhi ikionekana kutokuwa na uhusiano na shule kama vile mchango kwa wafungwa (Tshs. 100/- katika shule moja) au kwa huduma za afya (Tshs. 5,000/- kwa shule nyingine). Michango mingine hutofautiana sana kama mchango wa walinzi wa shule kiwango kidogo kikiwa Tshs 400/- kwa kila mtoto kwa mwaka mpaka kufikia Tshs 2,400/-. Michango mingine ni ya fedha taslim wakati mingine ilikuwa ya vitu kama kuni, mbolea au mboga za majani. Kwa mujibu wa watoto, baadhi ya shule zilikuwa zinataka michango mpaka aina sita tofauti, kuanzia michango ya dharura kama rambi rambi ya kuanzia Tshs 20/- mpaka Tshs 5,000/- watoto katika shule moja walikuwa wanakumbuka mchango wa ujenzi ambao ulikuwa unatakiwa kulipwa wote mara tu baada ya utafiti huu.

Utafti uligundua kuwa watoto walikuwa wanazuiwa kwenda shule wasipolipa michango hii. Watoto wa shule moja walisema kwa uhakika 'wasiotoa wanarudishwa nyumbani'. Katika shule nyingine wanafunzi walisema unaweza kuja shule kama umeshindwa kupata nembo ya shule, ambayo hupachikwa nje ya mfuko wa shati la shule, au ukishindwa kuleta kuni au jembe lakini usipolipa faini kwa uharibifu wa mali ya shule huwezi kuruhusiwa kwenda shuleni. Katika shule nyingine, watoto waliripoti kuwa usipolipa unaweza kupewa adhabu ya kuchapwa au kuchuchumaa kwa muda mrefu. Watoto 16 kati ya 29 wa sampuli ya watoto wakubwa katika shule moja waliwahi kuzuiwa kwenda shule kwa kutokulipa fedha kwa wakati fulani wa masomo yao. Watoto wadogo wa shule hiyo hiyo, waliripoti kuwa walitakiwa kuzuiwa wakati fulani kwa kutokuwa na nembo ya shule, lakini mara nyingi unaruhusiwa kwenda shule hata kama hauna nembo.

Kiasi kinacholipwa kwa masoma ya ziada, yaani nje ya muda wa masomo - maarufu kama twisheni - yanayotolewa na walimu, pamoja na malipo ya kila wiki au kila mwezi kwa ajili ya mitihani ya majaribio ni kikubwa. Kuna malalamiko mengi ya wanafunzi na wazazi kwamba walimu hufundisha vizuri katika madarasa ya masomo ya ziada ili kuwavutia watoto kuhudhuria.

Shule 4 kati ya 10 zilizokuwa kwenye sampuli wanatoza fedha kwa ajili ya masoma ya ziada. Shule ya mjini ilikuwa ghali kuliko zingine zote japokuwa ilikuwa katika eneo la watu wenye kipato kidogo. Katika shule hiyo watoto wa darasa la sita hulipa Tshs. 300/- kwa mitihani ya majaribio ya kila wiki zaidi ya kulipa gharama za twisheni ya Tshs. 200/- kwa wiki. Watoto 19 kati ya 25 walioko kwenye sampuli walisema hulipa tuisheni, jambo ambalo linaeleza kwanini watoto walio katika maeneo ya watu wenye kipato kidogo walisema kufaulu shuleni ni wajibu wao wenyewe.

Ili kupima kama hali inakuwa nzuri au mbaya zaidi, vikundi sita vilihitimisha kuwa michango ilikuwa mikubwa kuliko mwaka uliopita, vikundi sita vikasema imepungua huku vikundi sita vikisema hali ya michango iko vile vile (swali hilo halikuulizwa kwa vikundi viwili). Kwa bahati mbaya, kupungua kwa michango siyo lazima iwe ni kwa wale walio maskini - katika shule mbili michango ya fedha au vitu ilishaachwa kwa sababu mpango wa kutoa chakula shuleni ulishaachwa.

## 4.6 Je, Hali Inaboreshwa? Nini Kifanyike ili Elimu Iwe Bora?

Mabadiliko yanayobainishwa na utafiti huu katika shule za msingi yanatofautiana sana. Watoto tofauti walionyesha kuwa na vipaumbele tofauti, na kwa shule zingine watoto wakubwa hawakukubalina na wadogo zao kama hali inaboreshwa au inazidi kuwa mbaya. Kwa ujumla, vikundi kumi vilisema kuwa hali inaboreshwa, vikundi vinane vikasema hali inakuwa mbaya na vikundi viwili vikasema hakuna mabadiliko. Sehemu ambazo hali imeboreshwa ni kwa sababu huduma zimepanuliwa, kama za upatikanaji wa maji au uwepo wa komputa shuleni (Mwanza), au kwa mazingira ya ujumla na majengo ya shule. Pale ambapo walisema hali inazidi kuwa mbaya ilikuwa ni kwa sababu ya huduma ambazo zilikuwa zinatolewa, kama vile chakula shuleni, zimesitishwa mwaka huu wa utafiti au wanapaswa kulipia huduma za afya wakati awali zilitolewa bure.

Watoto walitoa mapendekezo tofauti 40 kuhusu njia za kuboresha elimu, kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la 3.

**Jedwali la 3: Mapendekezo ya Watoto Kuhusu Namna ya Kuboresha Elimu**

| Changamoto kwa Upande wa Wanafunzi (Upande wa mahitaji) | Ongezeko la Upatikanaji (Upande wa Upatikanaji) | Ubora katika Upatikanaji (Upande wa Upatikanaji) |
|---|---|---|
| Kusoma kwa bidii<br>Kuwasikiliza walimu/wazazi<br>Kuwa watiifu kwa wazazi<br>Kutokuwa watukutu<br>Kutokuwa watoro<br>Kuwa wasikivu darasani<br>Kufanya kazi za shule<br>Kuwasikiliza wakubwa zao | **1. Upatikanaji wa bidhaa za Shule**<br>Walimu zaidi<br>Madarasa zaid<br>Madawati zaidi<br>Penseli zaidi<br>Madaftari zaidi<br>Kalamu zaidi<br>Michango ya chaki<br><br>**2. Upatikanaji wa Huduma za Ziada**<br>Kama hawawezi kulipia, wapate tuisheni ya bure baada ya muda wa shule<br>Ujenzi wa zahanati<br>Usafiri wa bure<br><br>**3. Mtaala Uliobadilishwa**<br>Michezo zaidi shuleni<br>Masomo zaidi<br>Kuwa na mafunzo kwa vitendo, siyo nadharia tu | **1. Walimu Wazuri**<br>Kufundishwa vizuri (walimu kutokuwa watoro)<br>Walimu kuwajibika<br>Kupunguza adhabu kama njia ya kufundishia/kuwa na nidhamu<br>Wanafunzi kupewa nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu elimu<br><br>**2. Huduma Shuleni**<br>Kuongeza vyoo vya kudumu<br>Maji safi na salama<br>Upatikanaji wa hudumua ya afaya bure<br>Uwekaji wa madirisha<br>Ujenzi wa nyumba za walimu<br>Ujenzi wa maktaba<br>Kuweka umeme ili waweze kusoma usiku<br>Tengeneza vizuri mazingira ya shule kwa kupanda miti/kuweka bustani vizuri<br>Kuwa na viwanja vya michezo |

Sehemu kubwa ya mapendekezo inahusu kuongeza vifaa vya shule. Orodha ya kuongeza zaidi vifaa ('…zaidi') ilikuwa ndiyo msingi wa mapendekezo ya namna ya kuboresha elimu kwa vikundi 18 kati ya 20; isipokuwa Dar es Salaam ambapo msisitizo ulikuwa kwa wanafunzi kusoma kwa bidii na kuwa wasikivu kwa walimu.

Watoto wakubwa walikuwa na mapendekezo mengi kuhusu njia za kuboresha elimu - jumla ya mapendekezo yao inafikia 40 ukilinganisha na mapendekezo 26 ya watoto wadogo. Orodha yao iko makini na mahususi - huku watoto wa Dar es Salaam wakitaka mafunzo kwa vitendo na nadharia kwa masomo ya sayansi, na wale wa Rukwa wakitaka masomo mengine zaidi kama njia ya kuboresha elimu. Watoto wa Mwanza wanataka wapewe haki ya kuchangia mawazo yao kuhusu elimu. Wale wa Singida wanataka vifaa zaidi vya kujifunzia ili wasome hata nyumbani pia kwa muda wao wenyewe, na walimu wazuri zaidi watakaowasaidia wao kuelewa masomo. Ni dhahiri, kadri wanafunzi wanavyokua wanakuwa na mtazamo mpana kuhusu elimu bora na jinsi inavyoweza kupatikana.

Kama ilivyosemwa awali, watoto walio katika maeneo yenye kipato kidogo, hasa wale wa Dar es Salaam, wanasisitiza zaidi kwenye mahitaji ya kuboresha elimu, na nafasi ya watoto wenyewe katika kuboresha elimu yao. Dar es Salaam pia lilikuwa kundi pekee lililosema kuwa twisheni iwe bure kwa watoto wasiomudu kuilipia. Watoto pia walipokea vijitabu walivyopewa na watafiti, kwa hiyo picha ya ujumla inayojengeka ni ya hisia za kuwa na haki ya utoaji wa huduma kwa wote, wakiwemo wale ambao hawawezi kuilipia, pamoja na uelewa wa kuwa na bidii na kufanikisha masomo yao.

# SURA 5 Maoni ya Watoto Kuhusu Nafasi yao Katika Jamii

Kukua pamoja na kuwa na hisia za uraia ni mchakato wa kujifunza kupitia mahusiano ya vikundi vya kijamii ndani ya familia na baadaye ndani ya jumuiya kubwa. Zana za utafiti zilichunguza suala la nafasi au fursa ya watoto kwa kutumia mitazamo tofauti inayohusiana ili kuelewa mahusiano yanayoendelea. Watafiti waliuliza kuhusu:

1. Mchango wanaoutoa watoto kwenye familia na jamii zao,
2. Aina za taarifa wanazoziona ni muhimu na wanavyoweza kuzipata,
3. Njia mbalimbali rasmi na zisizo rasmi za kuwasikiliza watoto, na
4. Matarajio yao ya baadaye.

## 5.1 Watoto ni Wachangiaji Hai Kijamii na Kiuchumi

Ni wazi kuwa watoto, hata wale wa umri mdogo, ni washiriki hai kijamii na kiuchumi, wakichangia katika familia na jumuiya zao. Hii ilikuwa dhahiri zaidi Lindi, kwa kuwa baadhi ya watoto kwenye sampuli walikuwa wakuu wa kaya.

Watoto wadogo huchangia kwa kiasi kikubwa kwa kufanya kazi za nyumbani: kufua nguo, kuosha vyombo, kufagia, kusafisha, kupika n.k. mara nyingi kazi hizi huwapa watu wazima muda zaidi wa kujikita katika shughuli za kiuchumi na za kijamii zaidi. Watoto pia huwalea watoto wachanga, na huchangia kiuchumi kwa kuchunga mifugo (Arusha, Tanga), na kuuza katika maduka ya familia (Tanga). Watoto wanavyokua, kazi wanazofanya huongezeka, ikiwemo pia kuwaangalia wazee na kushiriki zaidi kwenye shughuli za kilimo na kuhudumia mifugo. Hata hivyo, watoto wakubwa wa Dar es Salaam walilalamika kuwa wavulana huwa wanakwenda kucheza badala ya kusaidia kazi za nyumbani jambo ambalo walisema siyo nzuri wakiashiria kuwa kazi za nyumbani zinatakiwa kugawanywa kwa wote, wavulana na wasichana, japokuwa hali haipo hivyo kwa sasa.

Watoto hufanya kazi nyingi shuleni, ikiwa ni pamoja na kulima shamba la shule au kuripoti pale ambapo mwenzao ametoroka shuleni. Pia kuna kazi nyingi ambazo hufanywa na wote, wavulana na wasichana, ili kuwasaidia walimu wao: kuteka maji, kuwapikia na kusafisha nyumba zao. Watoto wa shule moja walitaja pia kuandika ubaoni ili watoto wengine waone, wakimaanisha kuandika ubaoni kwa niaba ya mwalimu ili wengine wanakili badala ya mwalimu kufanya hivyo mwenyewe.

Aidha watoto huchangia katika ngazi ya jamii, mara nyingi, kama ilivyojitokeza kwa Shinyanga na Lindi, kwa kushiriki shughuli za ujenzi, kuleta maji na mchanga. Watoto wakubwa wanazidi kuchukua majukumu ya huduma katika jamii: kuwahudumia yatima (Shinyanga), kuwasaidia walemavu na kutoa huduma ya kwanza (Mwanza), kuwapeleka wagonjwa hospitali na kuwafundisha watu kusoma na kuandika (Rukwa), kuwasaidia wazee (Tanga), na kuwaelimisha wenzao kuhusu madawa ya kulevya (Dar es Salaam).

Wakati mwingine watoto huchangia katika kutoa maoni. Watoto wa Mwanza walielezea hili kwa kusema *'kutoa mchango wa mawazo kwa kila jambo linalostahili'.* Hata watoto wadogo wa Lindi walisema kuwa waliombwa kutoa maoni yao kuhusiana na kuuzwa kwa ardhi. Hata hivyo, wakati wanaweza kuulizwa kupendekeza bei ya kuuzia ardhi, walisema kuwa hawakuulizwa fedha zinazopatikana kwa mauzo hayo zitumikaje. Watoto wakubwa walisema wanawaelemisha wazazi na na jamii nzima juu ya mambo mbalimbali waliyojifunza kuhusu VVU/UKIMWI. Hata hivyo, kwa ujumla watoto wanadhani kuwa utoaji wa maoni au kushirikishwa katika yale wanayoyajua hupewa uzito mdogo ukilinganisha na kufanya kazi za nyumbani.

## 5.2 Taarifa Wanazozihitaji Watoto na Vyanzo Wanavyovitegemea

Kutokana na vikundi ishirini vilivyoshiriki katika utafiti, watoto waliainisha masuala 26 ambayo wanahitaji kupata taarifa. Watafiti waliripoti kuwa watoto wadogo na wale wa vijiini walikuwa na tatizo katika kuelewa swali hili wakati wa utafiti. Pengine hii ni kwa sababu unapokuwa unafahamu taarifa za kutosha ambazo

unazitaka, au unapoelewa taarifa hizo, unaanza kupuuzia zingine na hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kuamua taarifa gani ni nzuri au muhimu kwako. Ni ngumu kufikiria ni taarifa gani unazitaka wakati taarifa hizo hazipatikani au hujui kama zipo

Katika shule moja watoto wakubwa wa Mtwara walitaka kupata taarifa, lakini haikupatikana kwao. Hii ilihusu matumizi ya fedha za shule. Kwa kuzingatia matangazo mengi yanayosisitiza uwazi wa fedha za shule zinazopatikana na ushiriki wa watoto unaotarajiwa katika kamati za shule[16], taarifa hizi zilipaswa kuwa wazi kwa wote.

**Jedwali 4: Taarifa Wanazozihitaji Watoto**

Watoto wakubwa waliainisha masuala sawa na yale ya watoto wadogo. Masuala yao ya ziada yapo katika maandishi mlalo.

| Zinazohusu Elimu/Shule | Binafsi au za Kifamilia | Zinazohusiana na Jamii Nzima |
|---|---|---|
| Kusoma | Ndoa | Muziki |
| Kuandika | Mazishi | Kilimo / upandaji wa maua |
| Michezo / Burudani* | Matukio ya kifamilia mfano kifo | Michezo / Burudani* |
| Tratiba ya Shule / *Ratiba ya mitihani* | Afya / maradhi *- taarifa kuhusu HIV/AIDS, malaria, Homa ya Bonde la Ufa* | Wanyama wa porini wanaopita vijijini |
| *Masuala yanayohusu mazingira ya shule na mipango ya maendeleo* | | Ukosefu wa usalama ndani ya jamii mfano majambazi / maeneo yasiyo salama |
| | | Usimuliaji wa hadithi |
| *Kuandikishwa darasani*** | | Mikutano (mfano ya vijiji) |
| *Mashindano ya kishule* | | Kupata kazi |
| *Haki ya elimu* | | Habari |
| *- zikiwemo Matangazo mahususi ya Hakielimu* | | *- Pamoja na habari zinazotoka nje ya Tanzania* |
| | | *Programu za watoto* |
| | | *Mazingira* |
| | | *Kulima / kilimo* |
| | | *Wazee* |
| | | *Haki za mtoto* |

Angalizo: * Haikubainishwa katika muktadha huu iwapo watoto walikuwa wanamaanisha michezo ya shule au mechi rasmi kati ya timu zinazofahamika na hivyo iwapo michezo/burudani iwekwe chini ya taarifa zinazohusu shule kama sehemu ya taarifa ya jamii nzima.

** Siyo kila mmoja hupata nafasi ya darasa la kwanza moja kwa moja, wazazi wanatakiwa kuwaandikisha watoto wao ili kupata nafasi hii. Shule hutoa muda maalum wa kusajili wanafunzi, lakini kama taarifa hii haijulikana kwa wote baadhi ya watoto wanaweza kuachwa nje. Kwa kawaida ni watoto wa wazazi ambao hawafahamiani na watu wengi na kwa ujumla hawashiriki katika masuala ya jumuiya.

[16] Kamati za Shule ni sehemu ya sera na taratibu za taifa; zinawahusisha wazazi, baadhi ya walimu pamoja na walimu wakuu. Kwa utaratibu wa sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ni mweka sahihi katika akaunti ya benki na hivyo anaudhibiti wa fedha zinazotolewa katika ngazi ya shule na jinsi zinavyotumika. Mara kwa mara, mathalani wakati MMEM ulipoanzishwa, kumekuwa na jitihada za kuhakikisha watoto wanakuwa wanachama wa kamati za shule, lakini hii imekuwa ikipingwa na baadhi ya watu wazima ambao hawataki kuwa sawa na watoto katika kamati hizo.

Jedwali hili linaonyesha kuwa watoto wakubwa wanataka kupata taarifa zaidi na za aina tofauti. Ni dhahiri kuwa msisitizo mkubwa unahusu taarifa za shule, hasa kwa watoto wakubwa, pengine kwa sababu baadhi katika kundi hilo walikuwa wanakaribia mtihani wao wa mwisho, hivyo kuipa shule kipaumbele. Watoto wa vikundi vyote viwili vya umri wanalenga kwenye taarifa zinazohusu afya na jinsi ya kuepuka maradhi, pamoja na habari za kifamilia hasa za vifo. Watoto wakubwa pia waliweka kipaumbele taarifa zinazotoka nje ya Tanzania, taarifa za kulima na mazingira. Katika shule moja, mtoto alitaja taarifa zinazowahusu wazee - pengine ni kwa sababu ya utambuzi wa majukumu yake au ya watoto wengine; na mtoto mwingine alitaja haki za mtoto.

Kupendelea taarifa za kilimo na mazingira inaweza kuhusishwa na utambuzi wa shughuli za kujipatia riziki na maisha baada ya shule. Hata hivyo, inashangaza kuwa, licha ya taarifa kuonekana kuwa ni za muhimu kwa watoto kwenye vikundi vya majadiliano mkoani Arusha, Lindi, Mtwara, Iringa na Shinyanga, jumla ya watoto kumi na sita tu walikuwa na mawazo ya kuwa wakulima, na 12 kati ya hao walikuwa ni wasichana wa kikundi cha watoto wakubwa wa Mtwara.

Vyanzo vya habari pia vinadokeza mambo mengine. Watoto wakubwa hupokea taarifa kutoka kwenye vyanzo vingi kuliko wadogo zao.

**Jedwali 5: Vyanzo vya Habari Vilivyotumika na Watoto**

| Chanzo cha Habari | Ilitajwa na Wenye Miaka 7-10 | Ilitajwa na Wenye Miaka 11-14 | Jumla ya Kutajwa* |
|---|---|---|---|
| Radio | 5 | 5 | 10 |
| Kuambiwa na walimu | 3 | 5 | 8 |
| Televisheni | 4 | 2 | 6 |
| Kuzungumza na wenzao | 2 | 3 | 5 |
| Simu / simu za mkononi | 1 | 4 | 5 |
| Barua | 0 | 4 | 4 |
| Magazeti | 0 | 3 | 3 |

Angalizo: * “Jumla ya kutajwa” ina maanisha jumla ya idadi ya watoto katika vikundi maalum waliotaja kutumia chanzo hicho cha habari.

Vyanzo vifuatavyo vya habari vilitajwa mara moja au mbili na watoto: 'mitaani', kuambiwa na jamaa, kompyuta, mbao za matangazo, vitabu, mikutano ya vijiji, gwaride la shule (mstarini), vipeperushi, viongozi wa kijiji, mabango ya matangazo barabarani na matangazo kwa umma.

Watafiti walijaribu kuuliza iwapo watoto hupata taarifa wanazozihitaji wakati wanapozihitaji. Watoto wengi walisema kuwa walizipata, lakini kulikuwa na dalili za kukatishwa tamaa na upatikaji wa taarifa hizo. Katika shule moja, watoto walisema kuwa mengi ya wanayoambiwa na walimu yanahusu michango gani bado haijalipwa na lini inatakiwa, lakini hawapati taarifa juu ya lini walimu watatoa vitabu. Vikundi vingi vilisema hawakuambiwa kabla kuwa watafiti watakuja kuzungumza nao. Watoto wa Singida walilalamikia kwamba wanashiriki katika utafiti lakini hakuna mtu anayewapelekea mrejesho kuhusu matokeo ya tafiti hizo - suala ambalo utafiti huu utalipa kipaumbele.

Kitu mabacho utafiti huu haujafanikiwa kukibainisha ni kwa kiwango gani watoto ni wapokeaji tu wa taarifa/ maelekezo, 'kuambiwa na jamaa', 'kuambiwa na wazazi', na ni kwa kiasi gani huzitafuta wenyewe taarifa hizo, kwa kutafuta gazeti au kusoma mbao za matangazo. Watafiti pia hawakuweza kujua watoto hutumia fedha kiasi gani katika kupata au hata kuzungumza kuhusu habari, na hivyo ni kwa kiwango gani suala zima ni muhimu kwao.

## 5.3 Nani Huwasikiliza Watoto na kwa Nini?

**Usikilizaji Usio Rasmi**

Watoto waliulizwa maswali ya jumla kuhusu nani anawasikiliza, majibu yaokwa kiasi kikubwa yalitaja wanafamilia na jamaa zao na kwa kiasi kikubwa mazungumzo yasiyo rasmi. Watoto hawakuwataja walimu kuwasikiliza mpaka walipoulizwa njia rasmi za mawasiliano na ushiriki. Wazazi ni watu muhimu sana katika kuwasikiliza watoto, wakifuatiwa na wajomba na mashangazi. Mabibi na Mababu pamoja na watoto wenzao wanashika nafasi ya tatu. Watoto walipotoa majibu mahususi walisema kuwa mama husikiliza zaidi kuhusu masuala ya nguo mpya kwa ajili ya sikuu na baba husikiliza zaidi masuala yanayohusu elimu, kama vile kununua madaftari mapya japokuwa kwa Dar es Salaam watoto walisema kuwa mama husikiliza zaidi kuhusu masuala ya kusoma.

Sehemu kubwa ya mawasiliano kati ya watoto na wazazi wao inahusu masuala ya shule. Asilimia 55 ya vikundi vya utafiti walitaja masuala ya shule kama mada kuu ambayo wazazi husikiliza, wengi wakitaji upatikanaji wa vifaa vya shule, lakini watoto wa Dar es Salaam pia walisema pia kuwa huzungumza na wazazi kama wakifaulu mitihani, kama wakichapwa shuleni au kama wakihitaji fedha za twisheni.

Walipoulizwa kuhusu kwa nini walisikilizwa, majibu ya watoto yalitofautiana. Yanaainishwa hapa kwa kadiri ya vipaumbele, jibu lilitolewa mara nyingi likitangulia:

1. Kusikilizwa kwa masharti
   Watoto walisikilizwa kwa sababu wamekuwa na tabia zinazowafanya wao kusikilizwa. Kwa mfano: kama ukitumia lugha nzuri (Iringa), kama wewe siyo mtukutu (Dar es Salaam), kama ukiwa na bidii shuleni/una tabia nzuri/una nidhamu (Dar es Salaam na Mwanza - yote maeneo ya mijini), unapofanya jambo zuri (Rukwa na Mtwara), kama ukifanya unavyoambiwaa na wazazi (Rukwa) na kama ukiwaheshimu wazazi wako (Rukwa).

2. Kusikilizwa bila masharti
   Watoto walifikiri kuwa walisikilizwa kwa sababu wao ni wadogo na wanapendwa (Dar es Salaam, Lindi, Mwanza, Shinyanga), na ili wasaidiwe (Rukwa). Hii inaonekana kumaanisha kuwa baadhi ya watoto wana hisia za kusikilizwa bila masharti.

3. Kwa sababu wanatoa taarifa inayofaa
   Watoto huwashauri wazazi wao, na hivyo husikilizwa. Mifano iliyotolewa ni kwa wao kuzungumzia utunzaji wa miti (Tanga), au kuleta ujumbe kutoka kwa walimu (Mtwara). Sababu ya ziada ilikuwa ni kwa sababu wanakwenda shule (Rukwa), (ingawa hii inaweza kuwa sehemu ya kuwa na tabia nzuri).

4. Kwa sababu wana haki ya kusikilizwa
   Jibu hili lilitolewa na watoto wakubwa katika maneneo matatu - mawili yakiwa ya watu wenye kipato cha juu na kingine ni la eno la watu wa kipato cha kati. Hii inaashiria kuwa dhana zinazohusu haki hazishikiliwi na watu wote.

**Usikilizaji Rasmi**

Watoto waliulizwa pia kuhusu njia rasmi zilizopo kwa ajili ya kusikiliza maoni yao. Kwa familia, majibu yalifanana sana. Idadi kubwa ya watoto walisema wanasikilizwa na familia zao, hasa kuhusu masuala ya shule. Watoto wa Shinyanga walisema hii ni kwa sababu wakiwa wakubwa watawasaidia wazazi wao kama wakisomeshwa na kupata kazi nzuri. Watoto wadogo wa Arusha walikuwa na jibu tofauti - na Terat ni jamii ya wafugaji kwa ujumla - waliosema kuwa *'sisi tunaongozwa na wazazi'.*

**Kusikilizwa na Walimu**

Kuna walimu wanaowasikiliza watoto. Hii ni kutokana na kutajwa mara nyingi kwamba mwalimu mzuri ni yule anayeshauri (na hivyo inatarajiwa kusikiliza kwanza wanafunzi wanataka ushauri gani) na mwalimu anayesikiliza maelezo ya mtoto ya kwa nini amechelewa kuja shule badala ya kurukia tu kumwadhibu

mtoto kwa kuchelewa. Ni wazi kuwa walimu wa Tanga walikuwa wanafanya kazi ya ziada ya kuwaingiza watoto wasioona katika mfumo wa shule; na mafunzo yao ya tabia za aina hii yaliigwa na watoto - watoto walikuwa na shauku kuwa shughuli za utafiti hazitaanza kabla ya wenzao kuwa tayari kushiriki, wakiwemo wasioona.

Hata hivyo utafiti unaashiria kuwa hawa ni wachache. Vikundi vitatu tu kati ya kumi na nane (swali hili halikuulizwa Singida) vilisema walimu hujibu maswali darasani, wakimaanisha kuwa mawasiliano ni ya upande mmoja tu, kutoka kwa mwalimu kwenda kwa mwanafunzi na ndiyo njia waliyoizoea walimu wao. Dhana ya mwalimu kama tu anayesikiliza mwanafunzi ni ngumu kuiweka pamoja na adhabu ya viboko, kutokuwepo kwa mjadala kuhusu masula ya nidhamu, na kutokuwepo kwa baraza la shule, baraza la wanafunzi au njia zingine za kuwasikiliza wanafunzi, ambayo itajadiliwa katika sehemu inayofuata.

Walimu wengi wanaonekana kushikilia mtazamo wa wajibu na madaraka yao kwa watoto, ambao hauwezi kujadiliwa wala kuhojiwa, na wakati huo huo kusikiliza na mawasiliano ya pande mbili hayajitokezi kama vipengele muhimu vya mchakato wa mawasiliano. Hii inaonyeshwa na mitazamo katika baadhi ya shule kuwa hakuna haja ya kuwasiliana na wazazi kuhusu utafiti huu katika kuwahusu watoto wao, uhuru wa walimu kuwapa watoto kazi za ndani katika nyumba za walimu na ushahidi kwamba baadhi wa walimu hawatimizi wajibu wao wa msingi wa kufundisha.

**Muundo wa Kitaasisi wa Kusikiliza Katika Shule**

Tukizichukulia shule kama taasisi zenye miundo rasmi ya kuwasikiliza watoto, kunaleta picha tofauti kulingana na maeneo, katika kikundi kizima cha mjadala wengine wanasema kuwa shule ina miundo ya kuwasikiliza, na wengine wanasema kinyume kabisa cha hali hii. Katika shule moja watoto huwachagua wawakilishi wao katika kamati ya shule na wanaweza pia kuzungumza katika baraza la shule[17]. Katika shule nyingine, watoto walioshiriki katika utafiti walikuwa wanawajua wawakilishi wao, japokuwa siyo sehemu ya kamati ya shule. Haya hivyo walihisi kwamba watoto hawasikilizwi, kwa sababu watu wazima hudhani kuwa wao ni wadogo sana[18].

Vikundi vitano kati ya tisa vya watoto wadogo walioulizwa walidhani kuwa shule yao huwasikiliza pamoja na kutoa mifano iliyotolewa hapo juu. Kwa Tanga kuna vikundi vya kujisomea vinavyowasaidia watoto wenye matatizo ya kuona na walimu huvisaidia vikundi hivi bila gharama yoyote ya ziada. Vikundi vinne vya watoto wakubwa walikuwa na hisia kuwa shule yao huwasikiliza huku kikundi kingine kikiwa kimegawanyika nusu kati yao wanadhani kuwa wanasikilizwa na wengine wanadhani hawasikilizwi. Aidha, kwa Tanga, japokuwa hakukuwa na uwakilishi rasmi, kuna kamati ya wazazi (tofauti na kamati ya shule), ambayo watoto walisema kuwa huwasilisha mawzo yao kwa walimu. Watoto wa Shinyanga walikubali kuwa wanasikilizwa kwa kutoa sababu malum kuwa kuna *'bunge la watoto'* ambalo liliwezesha ushiriki wao katika shughuli za shule na kuwasadia kujifunza haki za mtoto katika muktadha wa haki ya kusikilizwa.

Kwa ujumla ni sehemu mbili tu kati kumi na nane zilitaja ushiriki wa watoto katika kamati za shule, na katika moja kati ya hizo, kukiwa na kikwazo kuwa mawazo yao hayasikilizwi kwa ukamilifu. Shule nyingi hazina mabaraza kwa ajili ya kuhamasisha ushiriki wa watoto, na hata uchaguzi wa viongozi wa madarasa, au viranja, unaonekana kufanywa na walimu.

**Usikilizwaji Katika Taasisi zingine**

Hakukuwa na asasi zisizo za kiserikali (AZISE) au asasi za kijamii ambazo zingeweza kutoa fursa ya ushiriki katika jamii zilizotafitiwa. Fursa zingine kama za asasi za kidini hazikutajwa na watoto isipokuwa

[17] Baraza ni mkusanyiko ulio rasmi kwa kiasi fulani unaoitishwa katika baadhi ya shule. Jinsi mjadala unavyoendeshwa na kiwango cha uhuru wa kutoa mawazo hutofautiana kutoka shule moja hadi nyingine.

[18] Kama ufuatiliaji wa matokeo ya utafiti, watoto waliamua kufuatilia katika kamati baadhi ya masuala yaliyoibuliwa wakati wa utafiti wa Maoni ya Watoto. Hususan walilenga kwenye kuleta kuni shuleni kila jumatatu ili ziuzwe kwa ajili ya shule kujipatia kipato. Watoto waliona kuwa kuni hizi huuzwa kwa bei rahisi sana na kwamba hii haiheshimu juhudi zao na muda wanaotumia kukusanya kuni hizi. Zaidi ya hayo, watoto hawakuwa na taarifa ya fedha zinazopatika kutokana na mauzo haya zinatumikaje.

kwa Dar es Salaam tu. Hapa watoto wanashirikishwa kuchagua viongozi wa sala za watoto, na mapokezi ya mchungaji mpya. Kwenye msikiti watoto pia waliulizwa mchango wanaoweza kutoa katika ujenzi wa jengo jipya. Kwa maana hii, taasisi za kidini zinaonekana kutoa fursa ya wazi zaidi kwa ushiriki wa watoto kuliko shule. Hata hivyo sampuli ni ndogo sana kuweza kuamua matokeo ya jumla. Ingekuwa vizuri kujua kwa nini watu wazima wanazifanya taasisi hizi kuwa nzuri kwa watoto, kwa kuwa na shughuli nyingi zinazokubali mchango wa watoto.

**Hitimisho Katika Vipengere vya Usikilizwaji**

Tukihitimisha kutokana na majibu yao kwa watafiti, watoto wanataka kusikilizwa, na karibu wote walijibu ndiyo kwa swali la mwisho katika utafiti kuhusu iwapo watoto walifurahia kushiriki katika utafiti. Mfano mzuri ni watoto wa Singida ambapo watoto 25 kati ya 26 walisema kuwa walifurahia kuchangia mawazo yao. Sauti ya kutoafiki ilisikika ikidai kuwa *kurudisha chakula katika shule za msingi ni ndoto.* Hivyo kuzungumzia masuala ya chakula ni kupoteza muda. Walipoulizwa kitu gani hasa walikipenda, watoto walisema kuwa wanapenda siyo tu nyimbo, maigizo na michezo bali walitaja pia kuelimishwa, kushirikiana nao na kujifunza; kitu ambacho kinaonyesha kuwa ushiriki wao katika utafiti umekuwa pia mchakato wa kujifunza kwao. Inaonyesha pia kuwa watoto walioshiriki walifurahia mawasiliano ya pande mbili na kujifunza kwa njia hiyo.

Taswira ya ujumla ni kwamba mawasiliano kama hayo ya pande mbili hayapo katika mahusiano yao na watu wazima. Watoto mara nyingi huwa wapokeaji tu wa taarifa, wakiambiwa badala ya wao kujishughulisha kutazitafuta. Inaonekana hakuna kiungo kizuri kati ya taarifa inayotolewa na kitendo cha kuwasikiliza watoto. Inaonekana hawatiwi moyo kufanyia kazi na kujishughulisha na taarifa hiyo na kutolea maoni, lakini kama wakitoa hoja, kwa masuala madogo madogo, kama vile iwapo wanahitaji daftari jipya, mzazi atatekeleza.

Shule hazijali matakwa ya watoto kwenye mambo wanayopenda na uwezo wao wa kushiriki katika taasisi, nje ya familia zao, hali ambayo huathiri moja kwa moja maisha yao ya kila siku. Ingawa wanachangia katika uchumi wa familia zao na jamii kwa kushiriki katika miradi ya ujenzi, kwa undani hali inaonyesha kuwa wapokeaji tu wa masomo wanayofundishwa, licha ya maoni mazuri wanayoweza kutoa kuhusu njia za kuboresha mchakato huo.

Watafiti wanahitaji kueleza zaidi kuhusu maatizo yaliyopo, hata hivyo, ieleweke kuwa watafiti walikaa na watoto kama wageni kwa muda mfupi. Kwenda ndani kwenye masuala nyeti zaidi kama vile iwapo na kwa njia gani mtu mzima husikiliza maoni ya mtoto yatima kuhusu nani wangependa kuishi naye, au jinsi gani wazazi wanalishughulikia suala la mwalimu anayetumia vibaya adhabu ya viboko, kunahitaji watafiti wawe wamekaa muda mrefu katika jamii hiyo na shuleni, kuhakikisha kuwa maswali wanayoibua hayamwachi mtoto akiwa katika hatari zaidi au kudhuriwa kuliko ilivyokuwa kabla.

## 5.4 Matarajio ya Baadaye

Baada ya kukusanya taarifa za maoni tofauti ya watoto kuhusu kusoma, na kuuliza nafasi ya watoto katika jamii, taarifa gani huwapendeza, nani anawasikiliza na mengineyo, watafiti walitaka kuwauliza watoto wanaonaje fursa zao za baadaye. Kuuliza swali, 'unataka kuwa nani ukiwa mkubwa?' ni jambo linalowafikirisha zaidi watu wazima kuliko watoto. Pia, tofauti kati ya kitu ambacho ungependa kuwa, na kitu unachodhani kuwa ndicho kitakachokutokea, ni ndogo sana kiasi kwamba wakati mwingine inakuwa ngumu, hasa kwa watoto wadogo, kuelewa. Kwa bahati mbaya muda haukuruhusu watafiti kuwauliza watoto kwa nini walichagua kama walivyofanya. Sehemu kubwa ya tafsiri inayofuata ni ya makisio.

Karibu kila eneo la utafiti liliweza kurudisha taarifa za jinsia ya mtoto pamoja na kazi wanazotaka kufanya. Ila kwa shule chache taarifa hazikupatikana.  Kwa kazi nyingi maarufu mgawanyo wa wastani ni kama unafuatavyo:

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 27

**Jedwali la 6: Matarajio ya Watoto Kuhusu Kazi**

| Kazi | Idadi ya Wavulana na Wasichana (Jumla 449) | Kati ya Wanaochagua Kazi Hii, % ni Wasichana |
|---|---|---|
| Daktari | 35 8% | 13 37% |
| Nesi | 38 8% | 34 89% |
| Rais | 39 9% | 13 33% |
| Mwalimu | 143 32% | 100 70% |
| Dereva | 18 4% | 1 6% |
| Rubani | 15 3% | 7 46% |
| Mwanajeshi/Polisi | 43 10% | 5 11% |
| Kuendelea kusoma | 10 2% | 2 20% |
| Mkulima | 16 4% | 15 93% |
| Sina hakika / waliochangua kazi nyingi | 8 2% | 7 88% |

Jedwali hili linawakilisha kazi zilizotajwa mara nyingi na hakukuwa na tofauti kubwa katika mgawanyo wa kawaida wa kazi kijinsia (ualimu na unesi). Hata hivyo, ni wazi kuwa rubani haikuonekana kuwa ni eneo la wanaume pekee, na kwamba mmoja kati ya watatu wanaotamani kuwa marais ni wasichana.

Matarajio ya watoto yanaweza pia kuchanganuliwa kwa jinsi wanavyojiweka katika soko la ajira na miundo ya utawala wa nchi.

**Jedwali la 7: Mwainisho wa Kazi Wanazotarajia Kuzifanya Watoto**

| Mgawanyo | Aina za Kazi Zilizomo | Asilimia (N=450) |
|---|---|---|
| Weledi/ za kulipwa mshahara | Madakatari, walimu, manesi, pia marubani | 54.9% (247) |
| Utawala | Rais, Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Wilaya / Wakuu wa Mikoa | 12.7% (57) |
| Ulinzi na Usalama | Jeshi na polisi | 10.4% (47) |
| Uzalishaji/nguvu kazi yenye ujuzi | Wafanyabiashara, mafundi (ufundi stadi, ufundi sanifu), wakulima | 9.3% (42) |
| Nyingine | Hii ni pamoja na watawala na mameneja kama wanavyoweza kuwa waledi/wa kulipwa mishahara katika huduma za serikali au 'uzalishaji'. Kundi hili pia linahusisha urembo, wachezaji wa mpira na makocha. | 6% (27) |
| Haijulikani / waliochagua kazi nyingi. | Pia inahusisha usista haikuwa wazi katika muktadha kama ina maanisha utawa au unesi. | 4.9% (22) |
| Wanafunzi | Aina yoyote ya kusoma zaidi (sekondari kwenda juu), lakini bila kuainisha kitu gani wangependa kufanya baada ya hapo. | 1.8% (8) |

Zaidi ya nusu ya sampuli ya watoto walipenda kuwa kwenye weledi wa mapokeo wa elimu na afya (kama madaktari au manesi), kukiwa na idadi kidogo ya wanasheria, pia na marubani kadhaa. Haieleweki vizuri kwa nini hii inakuja kwa nguvu hivi: inaweza kuwa ni kwa sababu watafiti walikuwa shuleni kwa hiyo watoto wakawa wanafikiria kazi unazoweza kuzipata kwa kusoma. Pia kuna uwezekano wa watoto kupendelea kuzungumzia zaidi mambo ambayo wangependa kuwa kuliko vitu ambavyo walifikiri watavifanya kwa uhalisia. Inaashiria mwelekeo mkubwa kwa kazi za weledi katika huduma, pengine kwa sababu kazi hizi zinafahamika kwa watoto zaidi. Kwa ufupi, mtu anaweza pia kusema kuwa wazazi wao wamewaona baadhi ya watoto kutoka kwenye jumuiya zao wakienda kwenye mafunzo ya ualimu na unesi, lakini wachache sana walioenda kusoma sheria, hivyo kunaweza kukawa na mitazamo kuwa sifa za kufuzu kwenda kusomea ualimu na unesi ni za chini ukilinganisha na sifa za kufuzu kwenda kusomea uwanasheria.

Kikundi kingine kikubwa, karibu 13% ni ya watoto wanaotamani kuendesha nchi. Madiwani katika serikali za mitaa hawajitokezi katika malengo haya, pengine kwa sababu hawa hawaonekani sana kwa watoto, ukizingatia wanapata taarifa kutoka kwenye redio, hivyo, habari za kitaifa zaidi. Vinginevyo, inaweza kuwa udiwani hauonekani kuwa ni kazi kama ilivyokuwa kwa mbunge.

Karibu 10% ya watoto, wengi wakiwa wavulana, wanapenda kujiunga na jeshi, polisi au mgambo.

Inaonekana wazi kwamba watoto wachache (chini ya 10%) wanatamani kufanya kazi ambazo zinaathri moja kwa moja ukuaji. Matarajio yanayobadilika ya watoto yanaweza kuwa ni ishara kwamba fikra kwa ujumla zinabadilika. Kama watoto wakiwaona watu wazima wanaowazunguka wanapata fedha kutokana na biashara, basi unaweza kutarajia kuwa watoto wengi zaidi wangependa kufanya biashara, lakini mifano mizuri ya hoja hii kwa vijijini ni michache na ipo mbalimbali sana, licha ya msisitizo katika ukuaji ngazi za chini. Hata hivyo, lazima kutakuwa na muda mrefu kati ya mabadiliko ya ukuaji wa uchumi/mabadiliko ya kijamii na mitazamo ya watoto kuhusu fursa zilizopo kwa ajili yao.

Hata kilimo, ambacho kiuhalisia itakuwa ni kazi ya baadaye ya watoto wengi wa maeneo ya vijijini, siyo chaguo lao la maisha ya baadaye. Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi, na kama kumekuwa na ongoezeko katika upanuzi wa kilimo, au fursa za masoko ya ndani kwa ajili ya bidhaa za kilimo, mtu anaweza kutarajia watoto hasa wakubwa kufahamu mambo haya, na kuziona kama maisha yao ya baadaye.

Inawezekana pia sababu ya wachache kuchagua kilimo ni kwa kuwa wapo shuleni, na kwa sehemu fulani ni kwa sababu watoto walidhani hakuna sababu ya kufikiria kwenda kwenye biashara kama utahitaji mtaji kufanya hivyo, na wao hawana uwezo wa kupata mtaji. Inaweza pia ikawa ni kwa sababu wanaona mifano michache sana ya watu waliofanikiwa kibiashara katika jamii zao.

# SURA 6 Hitimisho la Ujumla

1. Kuhusiana na methodolojia, kazi hii ilikuwa ya pekee sana kwa Tanzania, kuwauliza watoto maswali ya aina hii kwa mtiririko unaohusisha sampuli wakilishi ya nchi - licha ya sampuli kuwa ndogo ya watoto 500 tu. Kuna kujifunza kwingi kulikotokana na methodolojia na zana za utafiti kwa kazi za aina hii, hii ikiwa ni pamoja na kiasi cha muda unaohitajika katika mafunzo, na kwenye maeneo ya utafiti, urefu kwa ujumla wa zana za utafiti, na jinsi gani viwango vya kimataifa vya 'ridhaa ya kweli' vinaweza kutekelezwa katika maeneo ya mbali vijijini kukiwa na kiwango kidogo cha kujua kusoma na kuandika miongoni mwa wazazi. Taarifa za ziada kuhusu methodolojia zipo katika kiambatanisho cha kwanza.

2. Mitazamo ya watoto inaweza kuwa tofauti sana na ya watu wazima. Majibu yao kwa maswali yalionyesha kuwa wanatazama suala la kusoma na nafasi yao katika jamii kwa mapana yake, badala ya kuziona kama mada mbili tofauti na kwa namna ambayo watafiti watu wazima walivyoandaa zana za utafiti.

   Kwa upande mwingine, baadhi ya masuala ambayo watu wazima hutazama kama dhana moja, kama vile adhabu ya faini, watoto wanaiona kama mchango wa fedha - wakimaanisha kuwa nidhamu, na 'kufanya adhabu inayotolewa kuendana na kosa' siyo suala rahisi.

3. Kwa kutumia vigezo vikubwa, hoja kubwa ni umri wa watoto. Haishangazi, majibu ya watoto wakubwa ni tofauti kidogo, ni ya kina na yalionyesha kuwa wanafahamu mawazo mapya na wana uzoefu.

   Tofauti kubwa ya kipato, ni kwamba shule zote tatu zilizo katika maeneo ya watu wenye kipato cha chini ziliwasisitiza watoto wenyewe kuwa na bidii kama njia ya kujipatia elimu bora, wakati katika maeneo mengine yote kulikuwa na msisitizo mkubwa wa hitaji la kupata walimu zaidi, vitabu, majengo n.k.

   Tofauti za kijinsia zinajitokeza sana katika kazi ambazo watoto wangependa kuzifanya.

   Kigezo kikubwa cha kijiografia ni kati ya Dar es Salaam na maeneo mengine yote ya utafiti. Watoto wa Dar es Salaam wanapata taarifa zaidi na mawazo tofauti kutoka vyanzo mbalimbali, wana wigo mpana wa aina za kazi wanazotaka kuzifanya, na wana hisia zaidi za haki zao. Wao ni watoto pekee waliolalamikia walimu kuwatoza fedha za twisheni watoto wasio na uwezo wa kuzilipa, na pia walikuwa waungaji mkono wakuu kwamba njia za kuboresha elimu ni kwa watoto wenyewe kuwa na bidii zaidi.

4. Watoto wana maoni kuhusu masuala mengi yanayohusu kusoma, ambayo yanaweza kuwa ni mchango mkubwa katika mitazamo ya wakubwa na yanapaswa kuthaminiwa na wale wanaofanya kazi katika sekta ya elimu. Kutokana na umri wao wanaweza kuwa na mtazamo finyu kuhusu baadhi ya masuala - kama vile kiwango cha mchango unaotolewa na malengo yake - lakini kwa mengine kama umuhimu wa lishe au upatikanaji wa maji shuleni, na umuhimu wa mawasiliano kati ya shule na familia, ni wazi wana uelewa mpana.

5. Mawazo mahususi kuhusu kusoma shule yanayoibuliwa na utafiti huu ni pamoja na:

   a. Watoto wanaelewa umuhimu wa mazingira, katika mtazamo wake finyu wa 'mazingira ya kufundisha/kujifunza', na kwa masuala mapana ya mazingira yanayozunguka shule, upandaji miti na mengineyo.

   b. Kusoma kwao shule kunawafundisha umuhimu wa afya nzuri, lishe na maji safi huku kiuhalisia shule zinachangia kidogo sana kutoa huduma hizi muhimu.

   c. Kujifunza kunategemea sana kunakili maandishi kutoka ubaoni na kwenye vitabu vya kiada, japokuwa vitabu vinapendwa, na kwa baadhi ya shule vinaongezeka idadi, uhaba wa vitabu

vya kiada bado ni chanzo cha watoto kukata tamaa kwa sababu ni vichache sana. Watoto wengi wanatumia kitabu kimoja darasani, na wanakatishwa tamaa na kutokuweza kuvisoma kwa muda wao wenyewe.

d. Kuhusiana na walimu, kuna baadhi ya mifano ya vitendo vizuri sana na kujituma kwao, kama vile jitihada za kuwafanya watoto wenye matatizo ya kuona kuwa sehemu ya shule, na kwa ujumla, ni ishara kuwa baadhi ya walimu katika baadhi ya maeneo wanajitahidi sana kufundisha vizuri. Watoto wanajua vizuri mwalimu wanayemtaka: mtu anayetaka kweli kufundisha, anayewapenda wanafunzi, anabidii; na katika maeneo mengine hicho ndicho wanachokipata.

e. Kwa upande mwingine, walimu wengi wanaonekana kushindwa wajibu wao wa kimkataba. Kushindwa kuhudhuria darasani kulijitokeza kama tatizo. Viwango vidogo vya weledi wa walimu vinaonyeshwa na watoto, kama vile kuwapa watoto vitini bila kuelezea. Kanuni na taratibu za adhabu ya viboko hazifuatwi.

f. Kwa ujumla, mchakato wa kujifunza katika mazingira ya shule unaonekana kuwabana wanafunzi kufuata wanayoyasema walimu kama 'amri zilizowekwa' kwa ajili ya watoto ambao kwa kiwango kikubwa kazi yao ni kuzifuata tu. Mawasiliano kati ya shule na wazazi katika malezi ya watoto ni duni.

g. Michango ya hali na mali inatumika shuleni na watoto wanazuiwa kwenda shule wasipolipa.

h. Kulikuwa na maoni mbalimbali iwapo kwa ujumla hali ya elimu ilikuwa bora zaidi toka mwaka jana. Watoto wengi zaidi walionyesha kwamba njia bora zaidi ya kuboresha elimu ni kuongeza usambazaji wa nyenzo za ziada, ikiwa ni pamoja na miundombinu, walimu, na vifaa vya shule. Vilevile walitaka wawe na walimu bora zaidi, mtaala mpana zaidi, na huduma nyingine shuleni (kama vile huduma za afya). Watoto wa Dar es Salaam waliendelea zaidi kwa kusema kuwa kuongeza bidii yao wenyewe na kuwasikiliza walimu na wazazi itakuwa ni sehemu ya kuboresha elimu.

6. Hali ya ujumla ya watoto wanaokua inaonyesha kuwa wao ni washiriki wazuri kiuchumi na kijamii; na wanafanya kazi nyingi ambazo hunufaisha moja kwa moja familia na jamii zao, au huwasaidia watu wazima katika kuzifanya kazi hizo. Wanasikilizwa kwa njia isiyo rasmi na wazazi, lakini hisia za ujumla ni kuwa kuna mawasiliano duni - masula yanayohusiana na shule yalitajwa mara nyingi - inadhaniwa hii inaweza pia kuwa kwa vile utafiti ulikuwa unafanyika katika muktadha wa shule.

7. Watoto walionyesha kuwa kuna mambo mengi wanayoyapenda na hupata taarifa kutoka vyanzo mbalimbali. Licha ya nyumbani, mawasiliano ya kifamilia na ya ana kwa ana, radio ni chombo muhimu.

8. Usikilizwaji rasmi wa watoto katika taasisi ni duni sana. Walimu wanaoenakana kwa kiasi kikubwa kuwafundisha watoto kwa njia inayoanzia juu kuja chini: kazi yao ni kuelezea ili ujuzi wanaofundisha ueleweke, badala ya kuwawezesha kwa uwazi zaidi na kwa upana ili waelewe dunia wanayoishi. 'Kusikiliza' ni sifa ambayo haijitokeza kwa walimu licha ya kujibu maswali machache ya watoto wanayouliza darasani, japokuwa watoto katika shule moja walisema kuwa wangependa kutoa maoni yao kwa masuala yanayohusiana na elimu.

   Shule moja tu katika sampuli ilikuwa na baraza la shule. Katika shule chache ambapo watoto wanawakilishwa katika kamati za shule, mtazamo wa watoto ni kwamba hawasikilizwi vya kutosha; pale ambapo hawawakilishwi moja kwa moja, wanafunzi huwa hata hawajui siku ambayo mikutano inafanyika na nini kinajadiliwa. Sehemu pekee ambapo watoto wanashiriki vizuri na kusikilizwa ni misikitini na makanisani ambapo watoto wanapewa nafasi zaidi. Hata hivyo hili lilionekana katika eneo moja tu la utafiti. Hakukuwa na AZISE au asasi za kijamii katika maeneo ya utafiti, hivyo watafiti hawakuweza kujua kama hizi 'sekta' mpya huwapa watoto nafasi zaidi ya kusikilizwa.

9. Watoto wana matarajio mengi kwa kazi zao za badaye. Zaidi ya nusu walitaka kujiunga na kazi za huduma za elimu na tiba. Zaidi ya 10% walitaka kushiriki shughuli za uongozi wa nchi kwa njia fulani, kama rais, waziri, mbunge, mkuu wa mkoa au wilaya. Chini ya 10% walivutiwa na jeshi au ulinzi na tena zaidi kidogo ya 10% walitamani kujiunga na sekta ya uzalishaji kama wakulima, mafundi au wafanya biashara.

10. Ndani ya hoja hizi mahususi kuna ujumbe wa wazi. Watoto walifurahia kuwa sehemu ya utafiti, na kuona kuwa kutoa maoni yao ni kujifunza kwa jinsi ambavyo watafiti waliwauliza. Wakati mwingine, kama ilivyo kwa watoto wa Lindi (tanbihi ya 18), waliamua kuchukua hatua maalum na kuwajibika kwa mambo yaliyojitokeza katika mjadala, na ambayo yalionekana kwao kuwa siyo haki - wakionyesha jinsi gani kujifunza kwa pamoja na ushiriki mpana kijamii unavyoweza kukuzwa.

    Watoto wanaona vizuri mkanganyiko kati ya mtaala unaowafundisha umuhimu wa maji safi na lishe bora na wanachokipata shuleni. Mara nyingi maoni na hoja zao mahususi ni muhimu kwa watunga sera na watu wa mipango, na hii ni sababu ya kuendelea na aina hii ya utafiti wa 'Maoni ya Watoto' kwa namna endelevu.

**Zaidi ya hoja hizi za kiufundi, matokeo ya utafiti huu yana kipimo cha utu kinachowapa changamoto watu wazima wote, iwe wazazi na/au weledi: watoto wanataka kusikilizwa na kutambuliwa. Wanataka kufundishwa na walimu wanaopenda watoto, wanaopenda kufundisha na wenye bidii na hata kama ni katika kiwango cha kusikiliza tu maombi ya vifaa vya shule. Watoto wanataka na wanahitaji kusikilizwa.**

# KIAMBATISHO Maelezo ya Methodolojia

Kiambatisho hiki kinafupisha waraka mrefu zaidi unaojikita katika methodolojia ya utafiti huu, *'Maoni ya Watoto'.* Kinalenga fafanua tu jinsi kazi ilivyofanyika, ikizingatiwa kuwa utafiti shirikishi kwa watoto ni eneo linalokua Tanzania, na kwa kuamini kuwa wengine wangependa kuendeleza kazi ambayo utafiti huu umeianza.

## 1. Uandaaji wa Zana ya Utafiti Pamoja na Mafunzo kwa Watafiti

Zana ya utafiti iliandaliwa kwa njia shirikishi, ikiwahusisha wadau tofauti. Mada muhimu ziliainishwa kwenye mjadala na Kundi la Utafiti na Uchambuzi la Mfumo wa Ufuatiliaji wa Umaskini la Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na wale wanaofanya kazi katika utafiti wa *'Maoini ya Watu'* ambao ulikuwa ukifanywa na Kundi la Utafiti na Uchambuzi. Warsha ya watoto ilifanyika kupata maoni yao kuhusu mada zilizoainishwa, na ushauri wao wa jinsi ya kuanzisha mjadala kirahisi na kwa wengi kuweza kufikiwa.

Ufafanuzi kamili wa zana ya utafiti ulifanyika kwa muda wa wiki moja, wakitumiwa watafiti ambao tayari walikuwa na uzoefu wa kufanya utafiti na watoto[19]. Mafunzo zaidi kuhusu tofauti kati ya methodolojia ya utafiti unaohusu takwimu na ule unaohusu ubora yalitolewa. Orodha ya mada zilizojitokeza kwenye warsha ya watoto iliboreshwa ili kujikita kwenye masuala ya elimu/kusoma na pia kwenye nafasi ya watoto katika jamii. Hii iliboreshwa zaidi kwa kutengeneza maswali madogo madogo ya utafiti, huku maamuzi yakifanyika maswali gani yanauliza takwimu (yakitaka kujua idadi ya watoto wanaojibu ndiyo au hapana), na kwa yale ambayo watafiti watakuwa wanauliza ili kupata majibu yanayoelezea zaidi ubora (akiwapa watoto kujadili suala na kutoa mawazo yao), na yale maswali ambayo yana mchangiko wa yote mawili.

Maswali ya utafiti yalilinganishwa na zana husika kujua aina ya majibu ambayo watafiti wanatafuta. Msisitizo ulikuwa kwenye kuweka uchangamfu wa hali ya juu ili watoto waendelee kupenda kushiriki wakati huo huo wakihakikisha watoto wanajisikia salama na kulindwa, ili kama wakitaka kuelezea mtazamo unaopinga, au wakitaka kuibua tatizo hawatatishika au kujisikia kuwa katika hatari yoyote.

Mifano ya zana hizi ni pamoja na:

- Kwa maswali yanayohusu takwimu: *'Kuna walimu wa kutosha katika shule yako?'* (ndiyo au hapana). *'Hali imekuwa nzuri zaidi au imekuwa mbaya kuliko mwaka uliopita?'* (ndiyo au hapana). Majibu yalikusanywa kwa watoto kunyoosha mikono au kwa 'kupiga kura', kwa kutumia mbegu, mawe n.k - kitu chochote kilichopatikana katika mazingira yao. Katika maeneo mengine mchezo *'jua linang'ara'* ulichezwa. Watoto wanazunguka katika mduara na watafiti huuliza swali kama vile *'jua hung'ara kwa wale wanaolipa (au wasiolipa) michango ya shule'* na wale ambao kwao jibu ni ndiyo huja katikati ya mduara. Wawezeshaji wengine wanasimama nje na kuhesabu kwa haraka ni wangapi wanaingia katikati ya mduara kabla swali lingine halijaulizwa. Njia tofauti ni *'kuna nafasi katika basi kwa…',* na watoto ambao wangetoa jibu la ndiyo wanajiunga na basi katika muundo wa 'mamba'.

- Kwa maswali yanayohusu ubora: *'Nani anawasikiliza na ni katika masuala gani?'* Watoto walifanya maigizo ya mahusiano yao ya kila siku.

- Kwa majibu mchanganyiko: tofauti za maoni zilitumika. Mstari ulichorwa chini na watoto waliambiwa upande mmoja wa mstari ni walimu wapole, watu wanowasikiliza na kuwasaidia; na upande mwingine wa mstari ni walimu wanaosisitiza nidhamu, ambao mnawaogopa. Watoto wanaombwa kujiweka kwenye mstari kwa kadiri ya makisio yao ya walimu. Hii inatupa taarifa za idadi kama vile watoto wengi - 70%, wanawaona walimu kama watu wanaowasaidia badala ya watu wa kujenga nidhamu tu, pamoja na kuwezesha baadhi ya majibu ya ubora kwa jinsi watoto wanavyojadili miongoni mwao upande upi waende.

---

[19] Baadhi ya watafiti walipata mafunzo kuhusu utafiti shirikishi kupata taarifa za idadi kuhusu watoto katika warsha ya UNICEF: *'Participatory Approaches for Working with Children and Young People in Programme Planning, Implementation and Studies and Evaluation,'* Aprili 3 - 8, 2006, Dar es Salaam, iliyowezeshwa na Dynamix Ltd. ambayo pia ilihusishwa katika kutengeneza mwongozo wa zana za utafiti wa watoto nchini Tanzania, yaani *'Mwongozo wa Mbinu shirikishi: Ushiriki wa Vijana na Watoto'*

voc 30-9-08 :Layout 1  10/9/08  2:48 PM  Page 36

Maelezo zaidi ya aina hizi za zana yanapatikana katika *'Mwongozo wa Mbinu Shirikishi:* Ushiriki wa Vijana na Watoto' (2006) katika maktaba ya REPOA.

Rasimu ya zana ya utafiti ilijaribiwa na timu tatu za utafiti, kila timu ikiwa na watu wanne, katika shule tatu tofauti za Dar es Salaam. Kwa kurejea nyuma, muda mwingi ulipaswa kuelekezwa katika eneo hili la maandalizi ya utafiti, kwa sababu ya hitaji la kuhakikisha kuwa usawazishaji wa kutosha wa jinsi zana ya utafiti ingetumika katika kila kikundi katika timu tatu za utafiti.

Kanuni ya msingi ya utafiti shirikishi ni kwamba inaendana na mazingira husika, kiasi kwamba kama washiriki wakionyesha kupendelea suala fulani basi muda wa kutosha utengwe kwa suala hilo ili kulichunguza kwa undani. Watafiti walikuwa na ufahamu wa kutosha katika mbinu hii. Changamoto ilikuwa ni kuendeleza mlinganisho kwa kazi za vikundi vyote vitatu na hivyo kuweka kiwango cha usawazishaji. Hii ilikuwa ngumu zaidi kwa watoto kwa sababu, kama muda zaidi ukitumika kuchunguza suala husika kwa kina, muda wa kumaliza utafiti usingeongezwa kwa sababu watoto wangechoka sana au walitakiwa kurudi nyumbani. Watafiti hawakufanikiwa mara zote kupata usawazishaji unaotakiwa, ndiyo maana baadhi ya sehemu za utafiti hazikupata taarifa kutoka kwenye vikundi vyote ishirini vya utafiti.

Maboresho ya rasimu ya zana ya utafiti yalifanywa na viongozi wa timu za utafiti siku ya mwisho ya mafunzo, kisha muda ukatolewa kwa viongozi wa timu kuelezea mabadiliko machache yaliyofanyika katika timu zao kabla ya kazi kuanza.

## 2. Maadili ya Kufanya Kazi na Watoto

### Ushiriki

Watoto walishiriki katika kuandaa ajenda ya utafiti pamoja na kuwa washiriki katika utafiti. Katika kuandaa ajenda, watafiti walijaribu kutekeleza mambo mazuri yaliyoelezwa na wengi akiwemo 'Hart's Ladder[20], na uzoefu wa mafunzo yaliyofanyika REPOA kuhusu utafiti shirikishi kwa watoto[21]. Watafiti walikuwa wazi kwa watoto kwamba kiwango cha ushiriki ni kile ambacho wao wanatoa maoni, wanapewa taarifa na kuombwa ushauri kuhusu miradi au programu zinazotungwa na kuendeshwa na wazazi. Watoto walielezwa jinsi mawazo yao yatakavyotumiwa na matokeo ya maamuzi yanayofikiwa na watu wazima. Mfano wa suala ambalo vinginevyo lisingekuwa sehemu ya utafiti ni hitaji la watoto kujua iwapo watoto wanaelewa vitabu vya kiada.

Zana ya utafiti ilibuniwa kupata ushiriki wa hali ya juu kutoka kwa watoto, kupitia shuguli nyingi tofauti (za haraka, polepole, makelele, kimya, kuzungumza, kusikiliza, kuimba na mengineyo). Kwa kuzingatia mrejesho wa watoto (tazama sehemu 5.3 ya taarifa), walifurahia utafiti, na pia wanasubiri kwa hamu kuona mwendelezo wake.

### Maadili wakati wa Uwandani

Kama sehemu ya kazi katika maeneo ya utafiti, mafunzo yalilenga pia kuhakikisha kuwa angalau watafiti 'hawakusababisha madhara yoyote' kutokana na utafiti. Mmoja wa viongozi wa timu za watafiti aliongoza kipindi ambacho kilipangwa kuwafanya watafiti kutafakari visababishi vyote vya uhatarishwaji wa watoto, ikifuatiwa na kufikiria vizuri nini kifanyike ili kuepuka haya kutokea. Mifano ifuatayo ilihusishwa:

---

20 Roger A Hart (1997) *'Children's Participation: The theory and practice of Involving Young Citizens in Community Development and Environmental Care.'* Unicef /Earthscan. Hart alielezea njia ambazo watoto wanashirikishwa katika shughuli mbalimbali, kwa sehemu kubwa na watu wazima, na kuvipa majina viwango vya ushiriki kwa umhimu unavyopanda: udanganyifu/hila, mapambo, ushiriki mdogo, kupewa majukumu lakini hawajui, wanaombwa ushauri na wana taarifa, maamuzi yanayoanzishwa na wazazi na kuwashirikisha watoto, maamuzi yanayoanzishwa na kuelekezwa na watoto, maamuzi yanayoanzishwa na watoto na kuwashirikisha watu wazima. Watu wengi wamekosoa kazi hii, lakini ujumbe wa msingi wa watu wazima kujua wenyewe na kuwafanya watoto wajue kuhusu maana ya ushiriki, njia na sababu za ushiriki huo umebaki wazi.

21 Mafunzo ya utafiti shirikishi kwa watoto yalifanyika REPOA tarehe 13 - 19 Aprili 2005. Mafunzo yalifadhiliwa na Save the Children yaliwezeshwa na Deborah Wason, Rosemarie Mwaipopo na Derrick Mbelwa. Njia kadhaa shirikishi zilitumika kwenye mafunzo yakiwemo mafunzo kwa vitendo na watafiti wadogo.

- Watoto kupata matatizo nyumbani kwa kutokufanya kazi za nyumbani au kuchelewa kurudi nyumbani.
  Namna ya kuepuka: kuomba ruhusa ya wazazi ili watoto washiriki katika utafiti; kumaliza kipindi cha mjadala kwa muda uliokubalika.

- Wasichana kupata matatizo kwa kuonekana na 'wanaume wageni'.
  Namna ya kuepuka: kuhakikisha kuwa, kwa mfano msichana akitaka kuzungumza na mtafiti baada ya mjadala rasmi kunakuwa na mwanamke hapo.

- Walimu kujaribu kuuliza kwa watoto nani alisema nini katika utafiti, na iwapo kitu chochote kibaya kilisemwa kuwahusu wao au shule yao.
  Namna ya kuepuka: kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika mbali ili mtu aliye nje ya eneo la mjadala asiweze kusikia, kuhakikisha kuwa walimu wanaelewa kuwa taarifa zinazotolewa ni za siri na ripoti haitataja shule yoyote kwa jina, kuhakikisha kuwa watoto wanaelewa kuwa wanachokisema katika muktadha wa utafiti wasikiseme kwingine au kukirudia nje ya pale.

Kila mmoja wa watafiti alitia saini kanuni za maadili kwamba yeye atahakikisha kuwa hakuna madhara yatakayotokea kwa washiriki watoto. Nakala ya kanuni ilizotiwa saini iliwekwa katika faili la REPOA na nakala kuchukuliwa na watafiti.

**Ridhaa ya Dhati**

Kipengere kingine cha maadili kilikuwa kujaribu kuhakikisha kuwa wazazi wa watoto wamepewa taarifa sahihi kuhusu utafiti na wamepewa fursa ya kukataa kama hawakutaka watoto wao kushiriki. Watafiti walilenga kufanya hivi kupitia barua iliyotumwa kwa wazazi wa watoto baada ya watafiti kukamilisha uchaguzi wa washiriki kutoka kwenye kitabu cha mahudhurio ya wanafunzi. Kwa shule nyingi hili lilifanikiwa, na hakukuwa na wazazi waliokataza watoto wao kushiriki kwenye utafiti. Hata hivyo, katika shule moja walimu hawakutuma barua hizo kwa wazazi kwa sababu walisema ni jukumu lao kuchagua jinsi gani watoto wanatumia muda wao wakati wa saa za shule. Hivyo hakukuwa na haja ya kuomba ridhaa ya wazazi. Kwa shule nyingine mbili, barua zilitumwa bila maelezo mazuri kwa watoto na kwa wazazi ambao walikuwa na kiwango kidogo sana cha kujua kusoma na kuandika. Kilichotokea ni kwamba wazazi walifika shuleni siku ya utafiti, wakishikilia barua zao ambazo hazijafunguliwa na kuomba kutoa udhuru kwa ushiriki wao. Ni wazi hawakuelewa kuwa ilikuwa ni watoto wao tu ndiyo watafiti walitaka kuwaona, na walikuwa wamezoea kuwa kila ujumbe unaotoka shuleni ulikuwa ni wito wa kuitwa shuleni.

## 3. Utunzaji wa Taarifa na Uchambuzi

Mfumo ufuataao ulitumika kujaribu kuhakikisha kuwa na utunzaji mzuri wa taarifa wakati wa utafiti. Watafiti walishauriwa kufuata mchoro ufuatao katika muhtasari wao wa utafiti:

| Hoja Muhimu | Muhtasari wa Utafiti | Ufafanuzi / Maelezo |
|---|---|---|
| Sehemu hii hutumika wakati wa mchakato wa utafiti kwa mawazo yoyote ya mtu anayerekodi, k.v. watoto wanapata tabu kuelewa swali hili; watoto wanaanza kuchoka sasa; watoto wanaonekana wana hofu walipoulizwa kama walisikilizwa shuleni, n.k. | Sehemu hii hutumika wakati wa utafiti wenyewe - kurekodi yale wanayosema watoto (pia, kama inawezekana umri na jinsi ya mtoto), matokea ya kura, n.k.<br><br>Itakuwa haijapangwa vizuri na siyo nadhifu lakini ili mradi inasomeka, inatosha.<br><br>Sehemu hii ipo kwa Kiswahili | Sehemu hii hutumika jioni kuonyesha hoja muhimu, kuchukua nukuu zinazofaa n.k.<br><br>Hii inaweza kuwa kwa Kiingereza |

Ili kuepuka kupoteza maelezo ya kina, watafiti walitakiwa kutoandika tena mihutasari ya utafiti, na watafiti wenyewe walishiriki kufanya uchambuzi wa awali wa mihutasari kabla ya mchakato wa kuanza uandishi wa ripoti.

Uchambuzi wa kwanza ulifanyika kwa kuandaa ufupisho wa mihutasari ya utafiti kwenye makaratasi makubwa ambayo yaliandikwa katika mchoro ufuatao. Kwa kulinganisha safu mlalo na safu wima kuliwezesha timu ya watafiti kuona mielekeo inayojitokeza, maelezo yake ya kina yakichunguzwa kwenye muhtasari wa utafiti.

| Namba ya Swali (kutoka kwenye zana ya utafiti) na Umri wa Watoto | Mijini | Mchanganyiko | Vijijini |
|---|---|---|---|
| **Kipato cha juu** | Mwanza: Geita | Iringa : Mufindi | Lindi: Lindi Vijijini |
| **Kipato cha Wastani** | Singida: Singida Mjini | Mtwara: Mtwara Vijijini | Shinyanga: Maswa<br>Rukwa: Sumbawanga Mjini |
| **Kipato cha Chini** | Dar es Salaam: Kinondoni | Tanga: Tanga Mjin | Arusha: Arusha Mjini |

Kutoka kwenye uchambuzi huu hali ya ujumla ilijitokeza, kama ilivyoandikwa kwenye ripoti hii.

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 39

## 4. Mafundisho yaliyotokana na Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu 'Maoni ya Watoto' ulikuwa ni wa kujaribu methodolojia pamoja na matokeo yake. Kutokana na hili, yafuatayo ni mambo waliyojifunza watafiti:

1. Muda zaidi ulihitajika ili kuhakikisha kuwa zana ya utafiti iliyotumika inasawazishwa kuliko kuwafanya watafiti wapate uzofu tu katika njia shirikishi. Badala ya kuwa na timu tatu tofauti zikitumia zana katika maeneo tofauti, ingekuwa vizuri kufanya utafiti wote kama kundi moja kubwa, ili kupata makubaliano ya msingi ya jinsi kila zana inavyotumika.

2. Ushiriki wa watafiti wote katika kutengeneza mbinu ya utafiti ni wa muhimu, lakini gharama yake ni muda mrefu unaotumika kwa kila mmoja kutoa maoni yake. Kama ni kikundi kikubwa cha watafiti zaidi ya watu kumi na mbili waliotumika hapa, uwezekano ni kwamba isingefanikiwa. Ingekuwa vizuri kuwa na muda mfupi wa kazi ya kina zaidi kwa viongozi wa timu za watafiti, ikifuatiwa na mafunzo mahususi kwa watafiti kuhusu zana ya utafiti ambayo imeshatengenezwa na wahusika kukubaliana njia za kusawazisha zana hizo.

3. Mafunzo pekee yalichukua wiki moja, lakini siku sita mpaka saba zingetoa muda zaidi kuwawezesha watafiti kupata uzoefu wa kuchukua maoni ya watoto kwa maneno yao wenyewe. Ingekuwa vizuri pia kutumia vifaa vya ziada vya kurekodi, hususan, kamera na video.

4. Wakati mwingine watafiti walijaribu kuuliza maswali mengi zaidi, achilia mbali jitihada za kujaribu kuboresha zana ili kubaki na maswali ya muhimu tu. Ilionekana kuwa saa mbili mpaka mbili na nusu ni kikomo cha watoto kushiriki vizuri bila kuwa na mapumziko na viburudisho kidogo - jambo ambalo halikuwa kwenye bajeti. Kihalisia watafiti walikuwa katika maeneo ya shule/jumuiya kwa walau siku mbili mfululizo, hivyo ukiangalia nyuma ingekuwa vizuri kukutana na watoto mara mbili - siku moja kwenye suala la kwanza la elimu na siku ya pili kuhusu suala la pili la watoto katika jamii na kwa karibu saa moja na nusu kila wanapokutana.

5. Ingekuwa vizuri kutoa muda zaidi ili kujaribu kuchambua taarifa za utafiti kutoka kwa watoto na vyanzo vingine shuleni na katika jamii yao - hususan vitu kama gharama za kusoma. Gharama ya nembo ya shule (kama Tsh. 100/- tu) ilionekana kuwa ni kiasi kikubwa kwa watoto wengi, lakini watoto hawakutaja gharama za sare za shule, ambazo zingekuwa kubwa zaidi, (kwa mfano Lindi sare kwa mtoto wa darasa la kwanza inagharimu Tshs. 6,000/-). Ingekuwa vizuri kujua kama wazazi waliweka vipaumbele katika masuala ya gharama kama walivyofanya watoto, na kama ndivyo kwa nini au kwa nini sivyo.

## 5. Mapungufu ya Matokeo

1. Sampuli ilikuwa ndogo sana. Haieleweki vizuri kama matokeo ni shule moja mahususi au taswira ya mtazamo mpana zaidi wa wengi na uzoefu katika wilaya au mkoa.

2. Mbinu iliyotumika haikusawazishwa katika maeneo yote ya utafiti. Tofauti na hojaji ambayo swali huulizwa kwa maneno yanayofanana kwa kila mshiriki, njia shirikishi inahusisha kusema na kuelezea suala kwa maneno mengine na njia tofauti kuhakikisha kuwa watoto wameelewa. Kule Tanga, uwepo wa watoto wasioona kulifanya watafiti kuacha kutumia njia zote zinazotumia zana onyeshi.

3. Siyo kila swali katika zana ya utafiti iliulizwa katika kila eneo la utafiti. Hii ni kwa sababu ya suala la muda, kama muda ungetumiwa kuelezea suala ili kuwawezesha watoto kujibu, wakati mwingine watafiti waliishiwa muda wa kushughulikia masuala yote kama ilivyokuwa imepangwa. Hii ilimaanisha kuwa ni ngumu kufanya ulinganifu mahususi wa kiidadi kwa maeneo yote.

4. Matokeo yanasimulia hali zaidi kuliko kuelezea, na watafiti walibaki kushughulikia masuala ambayo vinginevyo yanahitaji utafiti zaidi, kama vile kwa nini watoto wa Dar es Salaam na Tanga walijikita katika kuboresha elimu kwa jitihada zao wenyewe, wakati sehemu zingine za nchi walijibu kwa kutoa orodha ya vitu wanavyovihitaji kama vile vitabu, walimu na vyumba vya madarasa? Kwa nini watoto wengi wanapenda kuwa walimu? Je, ni kwa sababu hiyo ni miongoni mwa kazi chache za mshahara ambazo wameziona? Kufanya kazi nzuri zaidi ya walimu wa sasa? 'Kulipiza kisasi chao' kwa watoto wengine? Isipokuwa katika hali isiyo ya kawaida ambapo watoto walitoa sababu zao, taarifa hazionyeshi sababu za uchaguzi wa watoto kuhusu kazi.

5. Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, watafiti walipata tu maoni ya watoto walioko shuleni. Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni 2.7% tu ya watoto wa umri wa kwenda shule ya msingi ndiyo hawako shuleni, na sampuli yote ya watoto 512 ingemaanisha kuwapata watoto 14 walioko nje ya shule kama wawakilishi wa wengine, au 1-2 katika kila eneo la utafiti. Hii inaonekana siyo haki kwa utata wa masuala yanayowakabili watoto walioko nje ya shule. Kuhakikisha kuwa sauti zao zinasikika ni changamoto kubwa kwa kazi za aina hii hapo baadaye.

Licha ya mapungufu haya, picha inayojitokeza inatosha kutuwezesha kutoa matokeo haya kwa kujiamini na kuwa na uhakika kuwa kuna mwanzo mzuri katika mchakato wa kujifunza kusikiliza maoni ya watoto wa Tanzania.

voc 30-9-08 :Layout 1 10/9/08 2:48 PM Page 41

# MAREJEO


Beecham, J (2001). *Involving Children and Young People in Planning, Implementation, Monitoring and Evaluation.*

Hart, R (1997). *'Children's Participation: The theory and practice of Involving Young Citizens in community Development and Environmental Care.'* Unicef / Earthscan.

Mascarenhas, O (2004). *What we know about Children in Tanzania based on a review of Studies.* REPOA.

National Bureau of Statistics (2007). *The 2007 Household Budget Survey.* Dar es Salaam.

Office of the High Commissioner of Human Rights (2003). *Convention on the Rights of the Child.* http://www.unhchr.ch/html/menu3/b/k2crc.htm. [Retrieved 23 January 2008]

Research on Poverty Alleviation (2005). *Report on Participatory Research with Children Training workshop* 13-19 April 2005, Dar es Salaam.

Research on Poverty Alleviation (2005) *Vulnerable Children in Tanzania and where they are.* Report to UNICEF.

UNICEF and Dynamix LTD (2006). *Workshop Report on Participatory Approaches for Working with Children and Young People in Programme Planning, Implementation and Studies and Evaluation,* April 3rd-8th, 2006, Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania and UNICEF (2006). *Mwongozo wa Mbinu Shirikishi: Ushiriki wa Vijana na Watoto.* Dar es Salaam.